# F.5 KISWAHILI-

## FASIHI YA KISWAHILI

## ORODHA YA VITABU VYA SILABASI MPYA YA KIWANGO CHA 'A' *(A-LEVEL);*

## P320/1 (UFAHAMU, NATHARI NA USHAIRI)

****Onyo: Usijibu zaidi ya swali moja kutoka sehemu moja.***

### SEHEMU A (Ufahamu)

Hapa kuna habari ya ufahamu maswali yake

### SEHEMU B (Nathari)

Hapa kuna matini au chopoleo yenye kutumia lugha wastani. Maswali yake yatahusu uhakiki wa matini hasa uchanganuzi ,fani ,umbo,muundo, mtindo, aina ya hadithi na lengo la mwandishi.

### SEHEMU CH (USHAIRI)

Ushairi kutoka makusanyiko mawili teule ambako shairi litateuliwa kwa kila diwani. Maswali ni mawili mawili. Chagua swali moja tu kutoka mojawapo ya diwani zilizoteuliwa. Diwani ni;-

1. Malenga wa karne moja………… Chiraghdin na Ahmed Sheikh Nabahany.
2. Malenga wa Ziwa Kuu ………………………… Walla bin Walla.

## P320/2; KARATASI YA PILI . TAMTHILIA;

***Onyo :Usijibu zaidi ya swali ya swali moja kutoka sehemu moja**

### SEHEMU A

1. Mabepari wa Venisi…………………………………………William Shakespeare.
2. Mfalme Edipode…………………………………………………… Sofokile.

### SEHEMU B

1. Kijiba Cha Moyo…………………………………………………Timothy M. Arege.
2. Kimya kimya kimya …………………………………………… Said A. Mohamed.

### SEHEMU CH

1. Mkwamo…………………………………………………Masereka Levi Kahaika.
2. Mizigo…………………………………………………………… John Ruganda.

### SEHEMU D

1. Kilio cha Haki ……………………………………………………Alamin Mazrui
2. Chema Chajiuza ……………………………………………Innocent Agume.

## P320/3; KARATI YA TATU. RIWAYA;

**Onyo**:Usijibu zaida ya swali moja kutoka sehemu moja.

### SEHEMU A

1. Utengano…………………………………………………… Said Mohamed.
2. Kiu ………………………………………………………Mohammed s. Mohamed.

### SEHEMU B

1. Nguvu ya Sala …………………………………………………… K. W Wamitila
2. Baraka za Mama…………………………………………… Vicent M Tweyambe.

### SEHEMU CH

1. Kufa Kuzikana……………………………………………………Ken Walibora
2. Uchungu wa Mwaridi…………………………………………Ndanda E. Antonio

### SEHEMU D

1. Uhasama Kilimani ……………………………………George Black Masereka.
2. Jitihada Zafua Dafu……………………………………………Wanyenya Willy.

***Onyo la jumla kuhusu karatasi ya pili na tatu.**

***Jibu Maswali matatu. Maswali Mawili yawe ya insha kutoka sehemu zilizo tofauti. Swali la tatu kuchaguliwa lazima liwe la aina ya Muktadha (dondoo) ambalo ni la lazima na litatokea sehemu yake pekee. Alama za kila swali la insha ni =33. kila swali la Muktadha ni =34.***

### VIPENGELE MUHIMU KATIKA UCHAMBUZI WA RIWAYA -P3 & TAMTHILIA –P2;-

1. **Jalada;** Ni gamba la juu ya kitabu.
2. **Anwani;** Ni jina la kitabu.
3. **Dhamira;** Ni lengo kuu la mwandishi katika kazi yake ya sanaa.
4. **Maudhui;** Ni **ujumbe** au mawazo mbalimbali ya mwandishi yanayojitokeza kitabuni.
5. **Wahusika;** Ni viumbe atumiao mwandishi katika kujengea au kuendeleza hadithi yake
6. **Mbinu/Fani;** Ni tamathali za semi anazozitumia mwandishi katika hadithi/kitabuni
7. **Mafunzo;** Ni maadili au mawazo yanayolenga kumwelimisha msomaji wa kitabu.
8. **Mandhari;** Ni mazingira/mahali panapotokea tukio katika jamii anayosimulia mwandishi.
9. **Ploti;** Ni mfululizo wa matukio kitabuni.

10. **Msimamo;** Ni hali ya mwandishi kuamua kufuata na kushikilia jambo Fulani. Katika vitabu vingi vya fasihi, msimamo wa mwandishi ni wa kimapinduzi dhidi ya kasoro zitendekazo katika jamii zetu za kiafrika anazotaka ziondolewe.
11. **Falsafa;** Ni mwelekeo wa imani ya msanii. Ni kile cha ukweli anachoamini mwandishi katika mazingira ya jamii yake.
12. **Mtazamo;** Ni jinsi mwandishi anavyoona mambo yakitendeka katika jamii yake.

## <u>BAADHI YA MBINU ZA KISANAA/FANI/TAMATHALI ZA SEMI KATIKA UCHAMBUZI WA FASIHI YA KISWAHILI;</u>

***Hizi ni Tamathali za semi zinazorejelewa katika uchambuzi wa kazi ya fasihi;***

**1. Semi/Nahau**; Ni maneno yenye maana fiche.

**2. Methali;** Ni maneno au sentensi kamilifu yenye maana fiche inayolenga kuelekeza tabia za watu katika jamii.

**3. Balagha/mbalagha**; Ni kuuliza maswali ambayo majibu yake ni bayana kwa muuliza swali.

**4. Koja/useja**; Ni mbinu ya mwandishi kuelezea kitu au hali kwa kutumia vitenzi vitupu kimoja baada ya kingine.

**5. Karaha**: kusema kwa kuonyesha chuki kubwa na mabezo *k.m.* mbona unakula bila kunawa?

**6. Inadi**: Hali ya kurudiana mtu jambo asilolipenda ili akasirke.

**7. Kijembe/ kilinge**: Aina ya fumbo linalokusudiwa kumpa ujumbe wa kumkasirisha, kumbeza anayeambiwa kumfanya ageuze msimamo wake, atende jambo la kumfurehisha aliyepiga kijembe hicho.

**8. Dhihaka;** Utani au mzaha.

**9. Kejeli/kebehi/stihizai**; Ni msingi wa maneno yanayosemwa kimafumbo yenye nia kumuudhi Yule anayeambiwa

**10. Kinaya ;** Ni kusema kinyume cha vile unavyomaanisha. Ni kusema kinyume cha matarajio.

**11. Hurafa;** kutumia wanyama kutenda kama binadamu katika hadithi.

**12. Udamisi;** Kutulia chumvi uwezo wa jambo kwa kuchagiza mtu kero au hasira KM;Sio mimi Aa! Ni wewe tu mwizi.

**13. Tawsira;** Picha ya akilini apatayo mtu baada ya kusoma au kutazama kitu fulani.

**14. Taharuki**; Hali ya masimulizi kuisha na Kumpa msomaji hamu ya kujua kilichofuata.

**15. Ritifaa**; Msemaji kuogea na kitu kisichokuwepo kifikira tu *k.m* kusifia mtu aliyekufa kana

kwamba yupo angali hai.

**16. Sira;** Aina ya riwaya inayosimulia maisha ya mhusika mkuu tangu utoto hadi ukubwani.

**17. Sitiari/jazanda**; Ni mlinganisho wa moja kwa moja bila ya kutumia vilinganisho K.M;Musa ni chui jihadhari naye .

**18. Tashihisi/uhaishaji/uhuishi**; Ni pale ambapo Viumbe hai au Vitu visivyo na uhai hupewa uwezo na sifa za binadamu. Kutenda kama binadamu.

**19. Shada:** Mkazo wa matamshi .K.M; dhahiri shahiri, Bure bilashi n.k..

**20.Nidaa;** Ni mbinu ya mwadishi kuelezea kwa kutumia vihisishi/maneno ya hisi .km; Alah!

**21.Kichapukizi:** Muziki unaoambatana na kitendo cha masimulizi.

**22.Mdokezo:** Kugusia habari bila kumalizia ali imaliziwe na mwingine . Mwingine amalizie kama anavyotaka .

**23.Tanzia;** Mhusika mkuu/wahusika wakuu katika hadithi hupatwa na masaibu makubwa na aghalabu huishia na kifo. Vifo vingi hadithini.

**24.Mkengeuko;** Kule kupingana na kanuni za msingi wa kijamii kwa kufanya kinyume cha vile unavyopaswa na kufuata yako mageni yanayokataliwa katika jamii husika.

**25. Tasfida;** kutumia maneno mateule yanayoficha aibu au matusi.

**26. Takriri;** Ni mbinu ya kurudiarudia maneno au kauli katika maelezo.

**27. Tabaini**; Ni mbinu ya mgongano baina ya mawazo. Km; Mweusi si mweusi, mfupi si mfupi.

**28. Tanakuzi**; Ni ukinzani kati ya falsafa na uhalisi wa mambo katika maisha ya mtu duniani.

**29.Taashira**; mbinu ya mwandishi kuelezea kitu au tukio kwa kutumia ishara Fulani.

**30.Tauria;** Mchezo wa maneno yanayofanana k.m. Wacha Yule Mhindi wa Bara Hindi apige miundi akanunue hindi aende Burundi.

**31.Majazi**;Ni mwandishi kumpa mhusika jina linaloambatana na maumbile, sifa na tabia zake

**32. Mafumbo**; Ni semi za maonyo au mawaidha zenye maana iliyofichika.

**33. Lakabu**; Ni jina la kupanga analobandikwa mtu kumpa sifa.

**34. Taniaba;** Hii ni mbinu ya kutumia jina la mtu binafsi kwa watu wengine wenye tabia au kazi sawa na mtu huyo. Km; Yesu wa kwanza wa Afrika, alikuwa Nkwame Nkrumah.

**35.Tanakali sauti;** Ni mbinu inayoonesha kuhusika kwa kitu kupitiliza Km; Kula fyuu!

Pia kuiga milio ya viumbe Km; Simba ananguruma grrrrrr! .

36. **Utohozi;** nimbinu ya kutumia neno kutoka katika lugha ya kigeni kama kiingereza na kuliendeleza kama neno la Kiswahili

## MBINU ZA UANDISHI

Mbinu ni njia ambazo mwandishi hutumia kufanikisha kazi yake.

**1.Uzungumzi nafsi**; Hapa,mhusika huzungumza na nafsi yake/mwenyewe/peke yake.

**2.Mbinu Rejeshi/kisengere nyuma**; ni mbinu ambapo mwandishi humrudisha msomaji nyuma ya vitushi baada ya kumpeleka mbele. Ili aweze kutambua zaidi juu ya yale yanayotokea kwa wakati husika.

**3.Kisengere mbele/ utabiri;** ni mbinu ambapo mwandishi hufikiria juu ya jinsi mambo yatakavyokuwa siku za mbeleni kutokana na kitendo Fulani.

**4. Ploti**; Ni mfululizo ya matukio kitabuni. Hapa mwandishi anapanga matukio kwa ajili ya kupanua kazi yake.

5**.Njozi/ ndoto;** ni mbinu ya kutumia maono yanayotokea katika fikra mtu anapolala hata anapopotelewa na fahamu. Ni mambo yanayotekelezwa kimawazo bila kuwa halisi au pia yanaweza kuwekwa katika uhalisia.

6.**Nyimbo;** hutumika katika tamthilia au riwaya ili kukamilisha ujumbe Fulani.

**7.Kuchanganya ndimi;** hutumika wakati ambapo msanii humfanya mhusika azungumze kwa lugha yake kwa mfano kiingereza au lugha ya kimama ambayo huwa tofauti na ile ya msanii. Hii ni katika hali ya kumkamilisha mhusika wake.

8.**Hadithi ndani ya hadithi/Mchezo ndani ya mchezo;** mbinu hii hutokea mwandishi anapobuni vijihadithi vidogo vidogo ndani ya hadithi kuu au michezo midogo midogo ndani ya mchezo mkuu.

9.**Halafa/Siunganishi;** ni mbinu ya uandishi kunapokuwapo na mfululizo wa vitenzi bila viunganishi.km Tulisafiri tukafika tukamwona akafurahi tukarudi.

10.**Kizimuo;** ni mbinu ya kutumia kichekesho au wimbo punde tu baada ya majadiliano juu ya wazo zito la kuch osha akili au jambo la ukinzani

11. **Ushairi;** Hapa mwandishi anatunga beti Fulani za mashairi katika kitabu chake.
12 . **Mdokezo;** ni mbinu ya kugusia habari bila kuikamilisha ilmuradi ikamilishwe na mwengine .k.m katikamatumizi ya kawaida ;
13 . **Kikengeushi;** ni mbinu ya kisanaa inayomfanya mtazamagi au msikilizaji asizugike na yale anayoyaona bali ayatafakari .
14. **Propaganda;** ni habari za uongo . mbinu hii hutumika kuwafanikisha wahusika waovu
15**.Sadfa**;ni pale ambapo vitendo viwili au zaidi vinapotendeka mara moja bila kutarajiwa wala kupangwa.
16 Upeo wa juu na upeo wa chini.
17. Taharuki

**P320/1**

**1. <u>UFAHAMU</u> 2. <u>NATHARI</u> 3. <u>USHAIRI.</u>**

**Mfano wa <u>NATHARI,</u>**

1. **Soma chopoleo ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;**

Hapo zamani za kale Abunuwasi alikwenda kuazima sufuria kwa jirani yake. Baada ya siku tatu hivi akairudisha sufuria hiyo pamoja na sufuria nyingine ndogo ndani yake. Jirani akazipokea huku akisema, “Hii ndogo si yangu; mimi nilikuazima hii kubwa tu” Abunuwasi akamjibu, “Hapana hata hii ndogo ni yako, kubwa ilizaa, na hii ndogo ndiyo mtoto wake.” Jirani akaastajabu sana kusikia kwamba sufuria imezaa. Lakini pia akafurahi kupata sufuria nyingine. Akamshukuru sana Abunuwasi, na akamwomba aje aazime sufuria zake wakati wowote.

Baada ya kama mwezi moja hivi, Abunuwasi akaenda tena kwa jirani yake. Akamwambia ana karamu na anahitaji kuazima kama sufuria tatu kubwa. Jirani akampa Abunuwasi sufuria haraka haraka kwa tamaa kwamba zitazaa tena. Abunuwasi akazichukua akaenda zake. Safari hii jirani wake akaona Abunuwasi amechelewa kuzirudisha sufuria; lakini akajipumbaza kuwa pengine zimo katika hali ya kuzaa mapacha. Wiki ikapita, wiki mbili, wiki tatu, nee, tano ahh! Sufuria hazijarudishwa. Jirani akaona afadhali aende akaziulizie.

Alipofika kwa Abunuwasi, akauliza habari ya sufuria zake. Akaambiwa kwamba sufuria zake zote zimefariki katika hali ya kujifungua, pamoja na watoto

wao; na kwamba yeye Abunuwasi ameshazizika na kizifanyia matanga. Jirani aliposikia hivi hamaki zikampanda. Akamwita Abunuwasi mwongo na mwizi, akidai kwamba ni muhali sufuria, kitu ambacho hakina uhai, kufariki dunia. Abunuwasi akamjibu, "jirani yangu, kumbuka kwamba kila kizaacho hakina budi kufa".

**Maswali;**

i) Hii ni ngano ya aina gani? Fafanua.

***Ngano ya Hekaya;*** *kwani ina* kisa kifupi kilichobuniwa kwa lengo la kubaini hekima.

ii. Chambua hadithi hii ukirejelea fani zifuatazo;

*a)* **Muundo**;

1–*Hadithi ina muundo wa moja kwa moja.*

*2. umeundwa kwa wahusika wawili wanaj; Abunuwasi na jirani yake.*

*3. Hadithi imeundwa kwa tukio la Abunuwasi kumwibia jirani yake sufuria*

b) **Mtindo –**

1. Mtindo wa Dayalojia.
2. Nafsi zote tatu zimetumika.
3. Ni ya aina ya Hekaya.
4. Mbinu kama; tashihisi

iii. Jadili mbinu za lugha zinazojitokeza katika chopoleo hiyo.

*1.**Tashihisi/uhuishi/uhaishaji;.** sufuria zimepewa uwezo wa kuzaa kana kwamba ni binadamu.*

***2.Methali;*** *kila kizaacho hakina budi kufa*

***3.mbinu rejeshi;*** *Hadithi nzima imejengeka katika mbinu rejeshi.*

iv. Ni nini msimamo wa mwandishi katika hadithi hiyo?

-*Matumizi ya hekima wakati wote.*

v. Eleza kwa tafsili matumizi ya mbinu ya Tashihisi.

-*Wanyama kuzungumza na kujibizana kama binadamu ni tashihisi.*

vi. Ngano hii inatoa maadili gani kwa watu katika jamii?

-Kuwa na hekima.

- kutumia busara wakati wote,

-kujihadhari na marafiki

## SEHEMU YA USHAIRI

## Vipengele muhimu katika uchambuzi wa mashairi

1. Dhamira
2. Maudhui

3. Muundo
4. Mtindo;
   -Aina katika shairi
   -Bahari katika shairi
5. Lugha;
   -mbinu/fani/tamathali za semi
   -uhuru wa kishairi/mshairi
6. Mafunzo/ maadili.
7. Toni ya malenga
8. Hisia za malenga
9. Urari katika shairi
10. Kuandika ubeti katika lugha nathari.

**<u>Sauti ya Dhiki ....Abdilatif Abdallah</u>**

**2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata;**

**Leo N'singekuwako**

**1. Kama tabu ni mauti,leo n'singekuwako**
**Ningekuwa ni maiti, 'mebakiza sikitiko**
**Ningekuwako tiyati, mtanga ndilo funiko**
**Leo n'singekuwako , kama tabu ni mauti**

**2. Hivi leo n'ngekuwa , kana kwamba sikuwako**
**Kitambo n'shafukiwa, nimo karibuni huko**
**Kungebaki kuambiwa : 'Atifu alikuwako.'**
**Leo n'singekuwako , kama tabu ni mauti**

**3. Marehemu ningekuwa , n'shaoza ni mnuko**
**Hawata kusumbuliwa,ni tabu na masumbuko**
**Na tabu haondokewa ,'ngenijiya niliko?**
**Leo n'singekuwako, kama tabu ni mauti**

**4. Kwa siku ngeliliwa , na jamaa waliyoko**
**Na maduwa kuombewa, nende salama nendako**
**Kisha hasahauliwa, kwa moyo na matamko**
**Leo n'singekuwako, Kama tabu Ni mauti**

**5. Na kwamba hata yakawa, hadi leo hawa niko**

**Ni kuwa huu moyowa, wahimili masumbuko**
**Ngeliya kwa yalikuwa ,hakika singekuwako**
**Leo n'singekuwako , kama tabu ni mauti**

***Maswali;***

i).Eleza Toni ya malenga katika shairi hilo.

- **Ni toni ya chini.**

ii).Eleza hisia za malenga katika shairi hilo.

- **Ni mwenye huzuni, majonzi, mawazo mazito.**

**iii).Chambua *uhuru wa kishairi* katika shairi hilo.**

- **Inkisari;** 'mebakiza,singekuwako,nende
- **Mazida;** maduwa, moyowa,
- **Tabdila:-** *'ngenijiya,ngeliya*
- **Kuboronga sarufi ;** *Marehemu ningekuwa*
- **Lahaja;** Mtanga, tiyati,

**iv).Eleza *Bahari* zilizomo kwenye shairi hilo.**

- *Bahari ya Ukara*
- *Bahari ya Mathnawi/manthawi*
- *Bahari ya kisarambe*
- *Bahari ya Sakarani.*

**v).Andika ubeti wa 3 katika lugha nathari**.

- ✓ *sarufi na maendelezo sahihi ya Kiswahili sanifu.*
- ✓ *Tumia aya moja badala ya ubeti husika.*
- ✓ Tumia  sentensi sahihi kisarufi badala ya mishororo.
- ✓ Usitumie vipande,vina wala mizani.Ujumbe uhifadhiwe.

**Vi). Ukirejelea shairi , eleza mtindo wake;**

(Mtindo ni sura ya ndani ya shairi. Hapa utoe aina na bahari zilizomo);-

- Aina ya ushairi ; ***Arudhi***
- Aina ya shairi;   ***Tarbia.***
- *Bahari ya Ukara*
- *Bahari ya Mathnawi/manthawi*
- *Bahari ya kisarambe*
- *Bahari ya Sakarani.*

**vii).Chambua Fani  katika shairi hilo;**

- **Kisengere nyuma;** Malenga anarejelea Shida / taabu alizozipitia
- **Takriri;** kibwagizo;- Leo n'singekuwako, kama tabu ni mauti.
- **Misamiati ya hali ya juu .**k.m; Mauti.
- **Taswira;** malenga anatujengea picha ya mateso ya dunia aliyopata Atif

| AINA | MISHORORO | |
|---|---|---|
| Umoja/tathmina | 1 | Tathmina au Umoja ni shairi lenye **mshororo mmoja** katika kila ubeti. |
| Tathnia | 2 | Tathnia ni shairi lenye **mishororo miwili** katika kila ubeti. |
| Tathlitha | 3 | Tathlitha ni shairi lenye **mishororo mitatu** katika kila ubeti. |
| Tarbia | 4 | Tarbia ni shairi lenye **mishororo minne** katika kila ubeti. Mashairi mengi ni ya aina ya tarbia. |
| Takhmisa | 5 | Takhmisa ni shairi lenye **mishororo mitano** katika kila ubeti. |
| Tasdisa | 6 | Tasdisa ni shairi lenye **mishororo sita** katika kila ubeti. |
| Usaba | 7 | Usaba ni shairi lenye **mishororo saba** katika kila ubeti. |
| Tumbuizo/Ukumi | 10 | Ukumi ni shairi lenye **mishororo kumi** katika kila ubeti. |

## BAHARI ZA USHAIRI

**Bahari za mashairi;**

Bahari katika shairi hupatikana kutokana na mpangilio wa;-

Vipande
Vina
Mizani
Wahusika
Maneno maalum
Mchanganyiko wa bahari kadhaa katika shairi husika . Hapa tunapata **bahari ya sakarani**

A) **Vipande;-**

kuna bahari tatu zinazopatikana kutokana na mpangilio wa vipande. Hapa lazima shairi lijichukulie bahari moja kati ya hizi tatu;-

**Utenzi**. Ni bahari ya shairi ambalo halina Vina vya kati. Pengine ni bahari ya shairi lenye kipande kimoja.

**Mathnawi / manthawi;-** Ni bahari ya shairi lenye vipande viwili katika kila ubeti , yaani ukwapi na utao.

**Ukawafi;-** Ni bahari ya shairi lenye vipande vitatu katika kila ubeti, yaani Ukwapi, Utao na Mwandamizi.

**B) Vina;-**

kuna bahari tatu zinazopatikana kutokana na mpangilio wa vina.

Hapa lazima shairi lijichukulie bahari moja kati ya hizi tatu;-

**Ukara;-** Ni bahari ya shairi ambalo vina vyake vya kipande kimoja vinahitilafiana au havifanani,huku kwenye kipande kingine shairi lina urari wa vina, yaani vina vinatiririka/vinafanana toka ubeti wa kwanza hadi ule wa mwishoni.

**Mtiririko;-** Ni bahari ya shairi lenye Urari wa vina katika kila kipande cha shairi husika, yaani kutoka ubeti wa kwanza hadi ubeti wa mwishoni.

**Ukaraguni;-** Ni bahari ya shairi ambalo vina vyake vinahitilafiana katika kila kipande cha shairi husika kutoka ubeti wa mwanzoni hadi ule wa mwishoni.

Ukaraguni ni kinyume cha bahari ya mtiririko.

4

**CH) Mizani;-**

kuna bahari tatu zinazopatikana kutokana na mpangilio wa Mizani.

Hapa shairi linajichukulia bahari moja kati ya hizi tatu;-

i) **Kisarambe;-** Ni bahari ya shairi lenye jumla ya Mizani kumi na sita (16) katika kila mshororo wa shairi husika. Vile vile, ni bahari

ya shairi lenye jumla ya mizani Nane 8 katika kila

mshororo wa shairi.

****Hapa, usizingatie mizani ya kibwagizo.**

ii) **Kikai;-** Ni bahari ya shairi lenye jumla ya mizani 12. Bahari hii ina mikondo kadhaa. Kwa mfano;- Shairi la BAHILI katika diwani ya

Sanaa ya Umalenga lina Mkondo wa 4 : 8. Mikondo mingine ya

Kikai ni;-

mkondo wa 8 : 4, na Mkondo wa 6 : 6.

iii) **Msuko;-** Ni shairi ambalo mizani yake ya kibwagizo imefupishwa sana, hailingani na mishororo mingine katika shairi husika.

**D) Mpangilio maalum wa maneno;-**

Kuna bahari zinazopatikana kutokana na mpangilio maalum wa Maneno.

Hapa lazima shairi lijichukulie bahari moja kati ya hizi tatu;-

**i) Kikwamba;-** Ni bahari ya shairi ambapo neno moja hutumika mwanzoni mwa kila mshororo wa beti za shairi. Huwa na mabadiliko ya maneno pia. Kwa mfano, shairi kuhusu 'maneno yenye maana zaidi ya moja' katika sanaa ya umalenga.

**ii) Pindu;-** Ni bahari ya shairi ambalo lina mchezo wa maneno na ina mikondo mingi. Shairi la pindu huchukua neno la mwishoni katika mshororo na kulifanya kianzo cha kipande au mshororo unaofuata. N.k…

**iii) Mandhuma;-** Ni bahari ya shairi ambalo ukwapi unapotoa wazo au swali , utao unatoa jibu lake.

**iv) Msemele;-** Ni bahari ya shairi lenye mafumbo . Hutumia lugha ya hekima kama vile , misemo/nahau, jazanda n.k..

5

**E) <u>wahusika;-</u>**

Kuna bahari zinazopatikana kutokana na mpangilio wa Wahusika katika shairi.

) **Ngonjera;-** Ni bahari ya shairi lenye wahusika wanaojibizana na Kujadiliana kishairi. Wahusika wanakuwa ndani ya shairi moja. Kwa mfano shairi la Binadamu na kasuku katika diwani ya Sanaa ya umalenga.

) **Malumbano;-** Ni bahari ya shairi ambalo mshairi anawasema au kuwahusisha washairi wengine kwa kuwatupia swali linalozua ubishi nao wakamjibu kwa kuandika mashairi tofauti.

BAHARI NYINGINEZO;-

**F) SAKARANI;-** Hii ni bahari ya shairi lenye mchanganyiko wa bahari nyingi ndani ya shairi hilo moja. Bahari hii ni ya lazima kwa mashairi yote yanayozingatia Ushairi wa Arudhi.

**G) Zuhali/Mavue;-** Ni bahari ya mashairi ya kisasa yasiyozingatia zile kanuni za utunzi wa mashairi kama vile;- Usawa wa mishororo katika kila ubeti, mizani, Vina na hata vipande.

**H) Sukui;-** Ni bahari ya shairi lizingatialo mizani na vina lakini si lazima ligawanyike katika beti au idadi sawa ya mishororo katika kila ubeti.

## UHURU WA MSHAIRI:

Malenga anao uhuru wa kutumia lugha kama anavyotaka kwa ajili ya kujenga fani, utimilifu wa mizani na Vina, pamoja na maudhui. Kwa hivyo, katika kunga zakee, malenga anaweza akatumia;- Inkisari,mazida,Tabdila,Kuboronga sarufi,Utohozi, kilahaja n.k…

**a) Inkisari;-** Ni kunga ya mshairi ya kufupisha au kuzibana baadhi ya silabi katika neno kwa ajili ya kupunguza na kusawazisha mizani au vina katika shairi lake. Kwa mfano;-

| **Neno;-** | | **Inkisari;** |
|---|---|---|
| Fuata | - | Fata |
| Niambieni | - | Naambeni |



**b) Mazida;-** Ni kunga ya Malenga ya kurufusha au kuzidisha sauti au silabi kwa ajili ya kuongeza mizani au kusawazisha vina katika shairi lake.

Kwa mfano;-

Neno;- Mazida;-

| | | |
|---|---|---|
| Moja | - | Mojamoja |
| Mwana | - | Mwanati |
| Sawa | - | Sawasawa |

**Tabdila;- N**i mbinu ya kulibadilisha neno kimatamshi kwa kuongezea herufi lakini bila ya kuongeza wala kufupisha mizani katika neno hilo.

Kwa mfano;-

| Neno;- | | Tabdila;- |
|---|---|---|
| Labda | - | Labuda |
| Dunia | - | duniya |
| Sharti | - | Sharuti |
| Mnajuta | - | Munajuta |

**Ch) kuboronga sarufi;-** Ni kunga ya kubadilisha miundo sentensi kisarufi. Hapa

Malenga hubadilisha sentensi ikawa kinyume na utaratibu wa kisarufi ufaao.

Kwa mfano;-

| Sarufi sahihi;- | | Kuboronga sarufi;- |
|---|---|---|
| Yesu atakuja | - | atakuja Yesu |
| Nilalapo kitandani usingizi siupati | - | kitandani usingizi nilalapo siupati |

**Utohozi;-** Ni kunga ya kulihotoa au kulitafsiri neno sisisi kutoka kwa lugha ngeni hadi kwenye matamshi na silabi za Kiswahili.

Kwa mfano;-

| Kiingereza;- | | Kiswahili;- |
|---|---|---|
| Time | - | Taimu |
| Member | - | Memba |
| Bye bye | - | Baibai |
| Cancer | - | Kensa |

**Kilahaja;-** Hapa, Malenga hutumia maneno kutoka lahaja zisizo za Kiswahili sanifu, katika shairi lake.

Kwa mfano;-

| <u>Lahaja</u>;- | | <u>Kiswahili sanifu;-</u> |
|---|---|---|
| Ndoo | - | Njoo |
| ufuase | - | Ufuate |
| Kitwa | - | Kichwa |

**Bahari za ushairi ni nyingi sana. Shairi huainishwa katika bahari fulani kulingana na mtindo wake, umbo lake na matumizi ya lugha.**

**Mifano ya Bahari za Ushairi**

1. **Utenzi -** shairi ndefu lenye kipande kimoja katika kila mshororo.
2. **Mathnawi -** ni shairi la vipande viwili (ukwapi na utao) katika kila mshororo.

*Ewe mtunga silabi, na sauti ya kinubi,*
*Majukumu hatubebi, maadamu hatushibi,*
*Mateso kwa ajinabi, kwa mabwana na mabibi*
*Ukija hayatukabi, karibia karibia*

3. **Ukawafi -** ni shairi la vipande vitatu (ukwapi, utao na mwandamo) katika kila mshororo.

*Nashindwa nikupe nini, nishukuru kwa malezi, mapenzi na riziki,*
*Ni pendo kiasi gani, lishindalo la mzazi, kweli mama hulipiki,*
*Ulinilinda tumboni, ukilemewa na kazi, ila moyo huvunjiki,*
*Kanilisha utotoni, mavazi pia malazi, ukitafuta kwa dhiki.*

4. **Mavue -** Shairi la vipande vinne (ukwapi, utao, mwandamo na ukingo) katika kila mshororo.

*Sisi walipa ushuru, wajenga taifa, tena kwa bidii, twahangaishwa,*
*Tumenyimwa uhuru, tuna mbaya sifa, hatujivunii, tunapopotoshwa,*
*Kila tunapopazuru, damu na maafa, hatutulii, hali ya kutishwa*

5. **Ukaraguni -** shairi ambalo vina vyake vya kati na vya mwisho hubadilika kutoka ubetio mmoja hadi mwingine.

*Vina Ubeti 1: ---ni, ---mi,*
*ubeti 2: ---ta, ---lo,*
*ubeti 3: ---po, ---wa,*

6. **Ukara -** shairi ambalo vina vya kipande kimoja havibadiliki kutoka ubeti mmoja hadi mwingine, lakini vina vya kipande kingine hubadilika. Kwa mfano, vina vya kati vinafanana kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho lakini vina vya kipande cha mwisho vinabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

   *vina Ubeti 1: ---shi, ---ma,*
   *ubeti 2: ---shi, ---ko,*
   *ubeti 3: ---shi, ---le,*
   *ubeti 4: ---shi, ---pa*

7. **Mtiririko -** shairi ambalo vina vyake vya mwisho na vya kati havibadiliki kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.

   *kwa mfano vina vikiwa ( ---ni, ---ka) kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.*

8. **Mkufu/pindu -** Shairi ambalo neno la mwisho au kifungu cha mwisho cha maneno katika ubeti mmoja, hutangulia katika ubeti unaofuatia.

   *Hakika tumeteleza, na njia tumepoteza,*
   *Nani wa kutuongoza, aliyepewa uweza,*
   *Filimbi akipuliza, tusiyeweza kupuuza,*
   *Bali twaisikiliza, bila ya kuzungumza,*

   *Bila ya kuzungumza, wala mwendo kulegeza,*
   *Tumwandame ja mwangaza, kututoa palipo giza,*
   *Penye dhiki ya kuliza, bila sauti kupaza*
   *Pengo hili kulijaza, ni nani anayeweza,*

9. **Kikwamba -** Neno moja au kifungu cha maneno hurudiwarudiwa kutanguliza mishororo au ubeti katika shairi.

   *Jiwe hili lala nini, ila moshi na majani,*
   *Jiwe linalala lini, litokapo vileoni,*
   *Jiwe hili halineni, lina macho halioni,*
   *Jiwe na tulibebeni, tulitupe mitaroni*

10. **Kikai -** Shairi lenye kipande kimoja kifupi (chenye mizani chache kuliko kingine) Mfano (8,4)

   *Nani binadamu yule, adumuye,*
   *Anayeishi milele, maishaye*
   *Jenezani asilale, aluliye,*
   *Kaburi liko mbele, sikimbiye.*

11. **Msuko -** Shairi ambalo kibwagizo/mshororo wa mwisho ni mfupi kuliko mishororo mingineyo. K.v (8,8) (8,8) (8,8) (8).

*Hawajazawa warembo, usidhani umefika,*
*Ukisifiwa mapambo, jinsi ulivyoumbika,*
*Akipata jipya umbo, 'tabaki kihangaika,*
*Usidhani umefika.*

12. **Mandhuma -** shairi ambalo kipande kimoja hutoa hoja, wazo ama swali, huku cha pili kikitoa jibu/suluhisho.
13. **Malumbano -** Mashairi mawili ambapo mshairi mmoja hutunga shairi akijibu au kupinga utunzi wa mshairi mwengine.
14. **Ngonjera -** Shairi lenye wahusika wawili wanaojibizana. K.m. Ubeti wa kwanza, mwalimu, na wa pili, mwanafunzi.
15. **Sakarani -** Shairi lenye bahari zaidi ya moja.
16. **Sabilia -** Shairi lisilokuwa na kibwagizo. Kituo (mshororo wa mwisho) hubadilika kutoka ubeti hadi ubeti.
17. **Shairi huru -** shairi lisilozingatia sheria za ushairi

**Shairi guni -** shairi lenye makosa ya arudhi za shairi

## UFAHAMU

UFAHAMU;

***1. Soma taarifa ya habari ifuatayo kasha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini yake:***

Takribani miaka thelathini iliyopita, karibu na mji wa Bombo paliishi mtu na mkewe waliokuwa wakipendana kama chada na pete. Punde tu baada ya kufunga *pingu za maisha,* Mungu aliwajalia matoto wa kike katika ndoa yao. Huyo ndiye aliyekuwa *kifungua mimba* katika aila hiyo. Baada ya mimba ya kwanza,Bi.kisakye alisita kuzaa na alikaa muda mrefu bila ya kupata nyingine. Hapakuwa na tama ya kupata mtoto mwingine, lakini baada ya miaka Kumi, kizazi kilifunguka na akazaa mtoto. Baada ya mwaka akazaa wa pili, wote wa kiume. Huyu mvulana wa pili ndiye alikuwa *kitinda mimba.* Maisha ya Bi. Kisakye hayakuwa marefu**.** *Punde si punde aliaga dunia* hii tamu mithili ya asali.

Bwana Mukasa ambaye kabaki mjane baada ya kufiwa mkewe, alikuwa katika masikitiko na huzuni *chungu nzima*. Hakuwa na furaha kamwe kwa msiba uliomfika, hasa alipokuwa akiwaona watoto wake wachanga wakiwa wagonjwa. Waswahili walipolonga ‘*Pang’okapo jino pana wasiwasi’* walisibu kweli. Familia nzima ilisikitika pakubwa.

Bwana Mukasa alimsisitiza binti yake, Monalisa, kuwatunza na kuwalea nduguze kwa malezi murua na mustahiki ambayo yangewafaidi katika maisha yao ya mustakabali kwenye jamii husika. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo na hivyo watoto wachanga hawa walifaa malezi mwafaka ili nao pia wawe wazuri ukubwani. Mara kwa mara Bw.Mukasa akimkemea binti yake juu ya malezi ya hao watoto kwani hakukuwa na mtu mwingine wa kuifanya kazi kama hiyo isipokuwa bintiye.

Monalisa –daka la mwana kabisa, mtoto wa adabu, mrembo, mcha mungu na mtiifu sana, aghalabu akiamka asubuhi na mapema mnamo mawiko ya jimbi la kwanza, na kujitayarisha kwa kazi za nyumbanimwao. Monalisa alikuwa na *bonge la kazi* mchana kutwa. Baada ya kuifagia na kuipiga deki nyumba yao, aliingia jikoni kuwapikia nduguze wadogo uji, wali na ndizi, na siku nyingine mhogo na viazi ulaya.

Msichana huyu alikuwa akipenda sana unadhifu kwani alipenda kuwalea nduguze wadogo kwa mwendo uo huo. Almuradi wawe wazima wa afya. Ilikuwa kawaida yake kuwaogesha asubuhi na mapema na kuwavisha nguo safi. Alipendelea sana nguo nyeupe pepepe! Kama theluji. Alikuwa mtiifu sana mbele ya babake na alikuwa tayari kumfanyia mambo mema bila ya bughudha zozote. Kama vile; Monalisa alikuwa akimpikia na kumpakulia pamoja na kukiandika chakula mezani. Isitoshe, akifua na kuzipiga pasi nguo za babake vizuri. Takribani kazi zote za nyumbani alizokuwa akizifanya marehemu Bi.Kisakye, zilikuwa zikiendeshwa na binti huyu Monalisa.

***Maswali;***

a) Pendekeza Mada mwafaka kwenye hadithi hiyo.

b) Hadithi hiyo ingeandikwa mwaka huu, unadhani babake Monalisa alimuoa mkewe mwaka gani?

c) Siku chache kabla mamake Monalisa kuaga dunia, kulikuwa na watu wangapi nyumbani kwao?

d) Toa maana ya methali '*Pang'okapo jino pana wasiwasi'* kama ilivyotumika katika habari;..

e) Eleza kwa tafsili tabia za Monalisa angalau Nne zinazoelezewa kwenye hadithi.

f) Fafanua wasifu wa Bw.Mukasa.

g) Taja na uelezee tamathali za semi au fani zozote za aina tano zinazojitokeza katika habari hiyo.

h) Eleza maana ya misemo ifuatayo kama ilivyotumika katika habari;..

i) Kufunga pingu za maisha.

ii) Punde si punde.

**1. Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata;**

*(Alama 20)*

Watu wengi hulinganisha adhabu na nidhamu .Wao huweka mipaka madhubuti ambayo ikikiukwa matokeo ni adhabu kali. Adhabu aghalabu hutolewa kama malipo kwa kosa likishatendeka. Je, kuna njia nyingine?

Dini hupendekeza kwamba kumuasa mwerevu ni bora kuliko kumchapa mjinga mara mia moja. Wataalamu wengi wanaashiria kuwa ikiwa ni lazima, basi kiboko kitumike tu iwapo njia nyingine zote zimeambilia patupu. Wanaamini kwamba kuchapa mara kwa mara hakubadili mienendo mibaya kuwa miema bali huendeleza dhana ya kwamba kosa ni kosa ikiwa litagunduliwa na adhabu kutolewa umuhimu wa nidhamu bila ya kukadiria adhabu iambatanayo na uvunjaji wa sheria.

Kufunza nidhamu kwafaa zaidi kabla ya, kuliko baada ya, tendo kufanyika. Ni muhimu, kwa mfano katika shule zetu, wanafunzi kuelezwa yanayokubalika na yasiyokubalika katika mazingira yao; kutilia mkazo umuhimu wa kutii na kutenda wema kuliko kutoa adhabu mtu anapokosa. Mambo mengine yaweza kufunzwa kwa kusisitiza manufaa ya kuwa na nidhamu bora. Kwa mfano,mwanafunzi akitenda wema,asifiwe na kuhimizwa kushikilia mkondo huo. Hili litendwe hadharani. Kwa upande mwingine, ukosefu wa nidhamu usipewe nafasi ya kunawiri bali ukomeshwe haraka iwezekanavyo. Wanafunzi,kupitia ushauri wa mara kwa mara,wahimizwe kujieleza kupitia kwa maneno badala ya hisia zao kudhihiri kupitia kwa matendo maovu. wahusishwe katika kuamua mambo yanayowahusu.

Kuna aina nyingi za adhabu iwapo itabidi tabidi tabia au matendo Fulani kukomeshwa lililo muhimu ni kwamba aelewe kuwa ametenda kosa na ni sharti aadhibiwe. Hasa ni muhimu adhabu ilingane na kosa. Mwanafunzi asiyekamilisha kazi yake darasani, kwa mfano ,aweza kunyimwa nafasi kushiriki michezoni kwa muda hadi kuwe na mabadiliko.mwanafunzi mchokozi aweza kutengwa na wengine ili aone umuhimu wa utangamano.

Adhabu ya kiboko karibu itapitwa na wakati na wakati, wasema baadhi ya wataalamu. Je, wanafunzi sugu wafanyweje? Upotovu wa nidhamu una mipaka yake. Mwanafunzi aweza kufukuza kwa muda kabisa ili kuwaokoa wengine shuleni. Nazi mbovu ni harabu ya nzima. Kwa upande wake, sarikali inapendekeza sana ushauri.ukosefu mwingi wa nidhamu hutokea kama njia ya mwanafunzi kutaka kudokezea hisia zake. Yafaa kufanywa uchunguzi kabla ya mwanafunzi kama huyu kuadhibiwa, isitoshe.kiboko kikitumiwa kupindukia, mwanafunzi hugeuka akawa kama sugu, haambiliki,hasemezeki. Kiboko kikikiuka mipaka,hudhuru badala ya kusaidia.

Maadamu nyakati zimebadilika, nidhamu na adhabu zitatekelezwa kama mambo mawili mbalimbali au waonaje?

**Maswali**

a) Pendekeza kichwa kinachofaa habari hii.

b) Kuna tofauti gani kati ya adhabu na nidhamu?

c) Taja njia mbalimbali za adhabu. Toa mifano kwenye taarifa,na mitatu yako mwenyewe.

d) Je,wanafunzi wachapwe viboko? Toa maoni yako

e) Methali " Nazi mbovu ni harabu ya nzima " ina maana gani?

f) Kamilisha methali hizi

i) Mtoto umleavyo …………………………………………………..

ii) Adhabu ya kaburi…………………………………………………..

g) Eleza maana ya ;

i) zimeambulia patupu

ii) kukiuka mipaka

iii) haambuliki hasemezeki

h) Taja tamathali za semi alizozitumia mwandishi katika habari.

1. **Soma taarifa ya habari ifuatayo kasha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini yake:**

Sisi vijana wa kisasa tuna jukumu kubwa la kujenga taifa letu. Katika kutetekeleza maendeleo nchini mwetu, lazima tuzingatie mawaidha au ushauri wa wazee wetu. Ni jambo la maana na muhimu sana kwetu vijana kusikiliza mashauri tunayopewa na wakubwa kama wazazi na walimu. Hii ni kwa sababu asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Kwa hivyo, tusipozingatia mawaidha ya wakubwa wetu, bila shaka huenda tukapotea njia na kufikwa shida au majanga makubwa kama yale yaliyompata kijana rafiki yangu Kadingo Ssempaata.

Hapo zamani katika kijiji cha Nakaseeta wilani Nakaseke, paliishi Mzee mmoja mkongwe na alijulikana kwa majina Mzee Dube Ssempaata. Mzee huyu pamoja na mke wake Muwajuma, walijaliwa na mtoto mmoja tu katika maisha yao. Ijapokuwa mtoto wa kiume huyo Kadingo alikuwa mwerevu sana masomoni shuleni kwao, alikosa nidhamu maishani mwake. Alikuwa mtundu sana. Alikuwa anawadharau walimu, wazee na hata wanafunzi wenzake. Alikuwa na kiburi si haba. Alijiona kwamba akili yake ingempeleka popote pale alipotaka kwenda. Kadingo alitenda mambo mengi mabaya; mara kachapa na kumjeruhi vibaya mwanafunzi mwenzake, mara kamtukana mwalimu wake darasani, kesi zake zilikuwa zikijitokeza kila siku. Kipindi hicho, Kadingo alikuwa anasoma kidato cha Nne. kwa hivyo, alikuwa miongoni mwa watahiniwa.

Siku moja Mzee Dube aliambiwa habari kuhusu visa na mikasa ya mwana wake. Aliambiwa kuwa mtotowake anavuta sigara na bangi, ana ushiririkiano na genge la wezi, anawatukana watu , nakadhalika… Haya yote aliyoambiwa Mzee Dube hayakuwa mageni hata kidogo. Mzee mwenyewe amewahi kumkuta bin yake na paketi ya sigara kwenye mfuko wa shati lake. Mzee alijaribu kuongea na mwanake, akamwonya na kumkemea mtoto wake aweze kuiacha tabia yake mbovu lakini wapi? Kadingo kayatia masikio pamba! Hakusikiliza chochote. Kwa kweli sikio la kufa halisikii dawa.

Kuna siku ambapo Kadingo alipatikana msituni akivuta bangi pamoja na vijana wengine katika genge lao. Punde si punde,Vijana hawa wote walipelekwa kwenye kituo cha Polisi hapo Nakaseke na kuadhibiwa vikali kwa kuchapwa viboko na askari-polisi. Walipigwa fimbo mfululizo kama matone ya mvua yanavyotoka angani yakianguka sakafuni. Askari waliwapa maonyo makali vijana hawa ili wasirudie kuvuta bangi na kutenda maovu katika jamii. Baadaye wakaachiliwa kurudi nyumbani kwao. Kumbe, Kadingo hakujifunza chochote kwa yoyote yaliyomfika kwenye kituo cha Polisi. Kadingo na genge lake waliendelea mbele na tabia zao mbovu za kuiba mali za watu, kupora simu na mikoba ya wanawake. Isitoshe, kuwaotea watu na kuwapiga mitaimbo wakati wa usiku.

Siku za mwizi ni arobaini, na hivyo, Kadingo alipatikana usiku wa manane na genge lake wakivunja na kupora pesa na bidhaa mbalimbali kwenye duka la mfanyabiashara maarufu kwa jina Bw. Byansi. Awamu hii, wanakijiji wa hapo hawakuchelewa kuchukulia sheria mikononi mwao, kwani walianza moja kwa moja kuwapiga wezi hao kitutu. Damu nyingi iliyowatoka kwenye majeraha makubwa waliyopata, iliwasababishia kuaga dunia papo hapo. Hatimaye, maiti za wezi hawa ikiwemo ile ya Kadingo, zilichomwa moto! Hayawi hayawi huwa! Kadingo na wenzake waliuawa kikatili kwa sababu ya kutenda maovu kadhaa. Na ni ukweli kwamba wanakijiji walikuwa wamechoka na tabia zao mbovu. Kweli, hasira hasara. Hii ndiyo maana waliamua kuwachukulia hatua ya kuwaua kwa sababu ya hasira chungu nzima walizokuwa nazo.

**Maswali;..**

a) Pendekeza kichwa cha habari mwafaka kwa hadithi hiyo.

b) Kadingo ni nani?

c) Eleza tabia za kadingo kulingana na habari hiyo.

d) Taja majina ya wazazi wa kijana huyo kadingo.

e) Kwanini Askari-polisi waliwakamata vijana watundu wanaotajwa kwenye habari?
f) ‘Siku za mwizi ni arobaini’. Eleza maana ya metheli hii ukirejelea mifano katika hadithi hiyo.
g) Taja methali zozote tatu alizozitumia mwandishi katika habari hiyo.
h) wanakijiji wa Nakaseeta waliamua kuwafanya nini vijana hawa baada ya kuwakamata wakiiba dukani?
i) Andika mafunzo angalau matatu unayopata kwenye habari hiyo.

**. Soma taarifa ya habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini yake;-** *(Alama 20)*

Mazingira ni jumla ya vitu vinavyomzunguka mwanadamu au kiumbe yule awaye katika mastakimu yake. Vitu hivi agahalabu huwa vya asilia kama mabonde, milima, mito,uoto, bahari na kadhalika. Baadhi ya vipengee vya mazingira pia vyaweza kuwa vilivyoundwa na mwanadamu kama vile majengo, barabara, mabwawa ya maji, vidimbwi na kadhalika. Kwa hali yoyote, mazingira ni kiini kikuu cha maisha yetu sisi wanadamu pamoja na viumbe wengine. Bila mazingira maisha hayawi maisha tena! Maisha hayawezi kustawi katika ombwe!

Mazingira, yawe ya asilia au yale yaliyotengenezwa na mwanadamu, ni nguzo ya utamaduni, dini, uchumi na hata ufundi. Kwa kiasi kikubwa mazingira huchangia pakubwa na hata pengine hushurutisha aina ya chakula, mavazi, makazi, dini na viwango vya ufundi. Kwa mfano watu waishio katika nyanda za juu wana maarifa ya kimapokezi ya kukabiliana na miinuko, milima, miteremko na mabonde. Wana ustadi wa kujenga maskani yao milimani na kujihami dhidi ya mimomonyoko ya ardhi. Hali kadhalika, watu waishio nyanda za chini na kwenye fukwe za maziwa na bahari huwa na ustadi wa kuogelea, ufundi wa kuunda vyombo vya maji kama vile mitumbwi na majahazi pamoja na uvuvi.

Mazingira bora ni mama yetu sisi wanadamu. Yatulisha na kutulinda tangu jadi na jadi. Jambo la kushangaza ni kwamba tumeamua kuyapiga mazingira mateke badala ya kuyashukuru kwa hisani zake. Tamaa imekuwa kiongozi wetu katika kuyaasi mazingira; tumekata misitu, tukatibua maji mitoni, maziwani na baharini kwa kutupa ndani mabaki ya uchakatuzi unaofanyika viwandani. Ardhi nayo imechafuliwa pasi mfano kwa kemikali kali zitumiwazo katika zaraa kukidhi maisha ya watu waongezekao kila kukicha duniani. Utengenezaji na utumiaji wa zana kali za kivita hasa mabomu ya kemikali na nuklia ni tishio kuu kwa mazingira yetu. Ama kweli sisi walimwengu ni kama *Juha Kalulu* akataye tawi analolikalia mtini!

Uchafuzi huu wa mazingira umeleta adhabu kali kutoka kwa mazingira: mazingira yameamua kulipisha kisasi kwa hali na mali! Ardhi imesusia kutupa chakula cha kutosha licha ya jitihada za kuilowesha kwa mbolea za wiwandani. Si nadra enzi hizi kusikia visa vya njaa na utapi wa mlo kwenye vyombo vya mawasiliano. Vimbunga kama vile *Katarina* kilichotokea kule New Orleans Marekani kilileta majonzi kutokana na vifo vya mamia ya watu pamoja na uharibifu wa mali inayokadiriwa kuwa mabilioni ya dola za Marekani. Uchumi wa mataifa mengi uko katika hatari ya kudorora kwa sababu sekta kama vile utalii zaathiriwa moja kwa moja kutokana na uasi wa

wanadamu dhidi ya mazingira. Kwa mfano hapa Afrika Mashariki ile theluji kwenye vilele vya milima Kilimanjaro, Kenya na Ruwenzori inayeyuka kutokana na ongezeko la joto duniani. Isitoshe, baadhi ya wanyama pori wanashindwa kuhimili hili ongezeko la joto na kuangamia pasi kuacha vizazi! Watoto na wajukuu wetu hawatapata kuona baadhi ya wanyama na hata mimiea tulionayo leo. Swala la uharibifu wa mazingira lazima litutie sisi sote kihoro kwa sababu sote tumo hatarini ya kuangamia; mabwenenye, makabwela, werevu, wajinga - kila hulka ya wanadamu! Jukumu la kila mmoja wetu ni kushiriki katika kusafisha mazingira na kuzuia uchafuzi zaidi. Maendeleo endelevu ni bora ili mazingira yetu yaweze kutukimu leo na hata karne zijazo. Tushiriki kuyatunza mazingira ili vizazi vijavyo navyo viishi bila sokomoko!

**Maswali:**

a) Ni nini maana ya Mazingira kutokana na mwandishi?

b) Taja vitu vitatu vya asilia vinavyounda mazingira.

c) Miinuko, milima na mabonde hupatikana katika nyanda zipi?

d) Kwa nini mwandishi anachukulia mazingira kuwa ‘mama yetu sisi wanadamu’?

e) Toa mifano mitatu inayodhihirisha jinsi mwanadamu anavyoharibu mazingira.

f) Eleza kwa ufupi matokeo yoyote mawili ya kuchafua mazingira.

g) Ni kina nani wamo hatarini kutokana na uharibifu wa mazingira?

h) Pendekeza mada mwafaka kwa taarifa hiyo.

.

i) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika habari.

i) zaraa ii) ardhi imesusia kutupa chakula cha kutosha iii) vilele vya milima

**Soma ibara ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata**.

Siku moja wakati wa siku ya wazazi shuleni kwetu tulishuhudia kisa cha kuhuzunisha sana. Siku hiyo kila mwanafunzi aliamka mapema akiwa na furaha na bashasha ya kukutana na mzazi wake au mlezi wake.

Basi kama ilivyo kawaida,wanafunzi walianza kufagia na kuokota makaratasi kwani tayari sehemu nyingi za shule zilikuwa zimenadhifishwa awali. Shule ilikuwa ni safi,inang’ara kwani majengo yote yalikuwa yameshapakwa rangi ya maziwa na kupigwa mkato wa rangi ya kahawia. Njia zote zilikuwa zimepangwa mawe ambayo yalirashiwa na kupulizwa chokaa nyeupe. Miti

nayo haikusahaulika,ilipakwa rangi nyeupe mle mashinani.Nyasi zilikatwa kwa urefu wa kimo cha nyoka na bustani kusawazishwa. Alimradi kila mahali palionekana pamwng'ara jinsi shule ilivyopambwa na kurembeshwa ungefikiri tulimtarajia Malkia kuzuru shule yetu.kwani hata yale magofu yaliyokuwa yamesahauliwa miaka nenda miaka rudi pia yalipakwa rangi baada ya kufanyiwa ukarabati.Walimu na wanafunzi walistaajabu, 'lo! Na pesa zote hizi zimetoka wapi?'

Baadaye wageni,wazazi,ndugu na marafiki walianza kuwasili na mwongoza tamasha ambaye alikuwa mwalimu wetu wa Kiswahili akatushauri tukusanyike mahali pamoja kupitia kwa kipaza sauti. Baadhi ya wageni walikuwa wamefika na kukaribishwa kwenye ukumbi ambao pia ulikuwa umejengwa mahsusi kwa sherehe hiyo.

Kipindi cha kuwatumbuiza wazazi na wageni kiliwadia. Tukajipanga kulingana na ratiba iliyotayarishwa awali.Vikundi vya awali vikatangulia kisha zamu ya Mwafia ikafika. Mwafia alikuwa kijana shupavu na mwerevu darasani lakini alikuwa hana afya nzuri na mara nyingi akivaa nguo chafu na kuchana kwa nadra nywele zake ndefu za kipilipli. Lakini ajabu siku hiyo alionekana mtanashati. Nywele zake kanyoa,zikawa fupi na nzuri.Alivaa sare mpya ya shule,akafunga tai na akavaa koti. Viatu viling'ara kushinda vya wanafunzi wengine wote.Wengine walisikika wakisema,Huyu si yule Mwafia tumjuaye! Lakini kama itakuwa hivi,siku za wazazi zije kila mwezi.

Japokuwa Mwafia aling'ara sana siku hiyo,afya yake ilikuwa bado ina dosari.Mwafia alipanda jukwaani ili kukariri shairi lake juu ya mahitaji ya wanafunzi shuleni.kufumba na kufumbua watu walimuona Mwafia amelegea na kuanguka chini kama gunia shinda huku akiweweseka na kuanza kuita ''Nyundooooo,Nyundoooo,Nyundoooo,….''Wanafunzi wenzake walimkimbilia na kumuondoa pale hadharani.Wanafunzi na walimu walijaribu kumpa huduma ya kwanza lakini hawakufua dafu,kwani Mwafia hakuamka.Punde wanafunzi walikumbuka ya kwamba Mwafia ana ''dawa''yake ambayo hubugia mara kwa mara. Hivyo basi mmoja wa maarifu wake alimita mwanafunzi mmoja kando na kwa siri akampa ''unga'' mchache.Mwanafunzi huyo alimpelekea Mwafia na kumnusisha bila ya walimu kuona. Mara tu Mwafia alipounusa ''unga'' ule alifungua macho na kutabasamu.Alipoanza kupata fahamu vizuri walimpa ule uliobaki akaubugia na kisha akaamka. Hivyo ndivyo ilivyokuwa mara ya mwisho kwa Mwafia kuonekana shuleni.

**Maswal**i

a) Taja sababu mbili zilizowafanya wanafunzi kunadhifisha kila mahali shuleni. alama 02

b) Eleza jukumu la Mwalimu mwongoza tamasha anayetajwa na mwandishi (alama 01 )

ch) Mwafia alipatwa na shida gani alipokuwa jukwaani? (alama 02)

d) Tambua sifa zezote nne za Mwafia (Alama 02 )

e) Kutokana na maelezo yako mwenyewe,unga aliopewa Mwafia ulikuwa unga gani? (Alama 01)

f) Kwa nini dawa aliyopewa Mwafia ilitolewa kwa siri bila kuonyeshwa kwa walimu? (alama 02)

g) Mwandishi ana maana gani anaposema,…hata yale magofu yaliyokuwa yamesahauliwa miaka nenda miaka rudi,’ ( alama02)

h) Kwa nini mwandishi alilinganisha ziara hii kwa ile ya kumtarajia Malkia? alama02

i) Toa sababu iliyowatamanisha wanafunzi kuwa na siku ya wazazi kila mwezi? (alama 02)

h) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika ibara.

i) ng’ara (alama01)

ii) mtanashati ( alama01)

iii) kufumba na kufumbua (alama01)

iv) hawakufua dafu (alama01)

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;**

Muziki ni burudani muhimu kwa binadamu hapa duniani. Kwa kweli Kuna waimbaji au wanamziki wengi sana katika nchi tano za Jumuiya ya Afrika mashariki. Wanamziki hawa wameimba nyimbo nzuri nyingi mwaka huu na ni vigumu sana kuamua au kuchagua wimbo mzuri zaidi ya nyimbo zote zilizozinduliwa mwaka uliopita. Kuna waimbaji wakubwa na waimbaji wadogo. Miongoni mwa waimbaji Watano wakubwa sana hapa Afrika mashariki mwaka uliopita kuna; Jose Chameleon, Diamond Platinumz, Sauti Sol, Bebe Cool na Eddy Kenzo. Waimbaji hawa wana nyimbo Chungu nzima. Nyimbo zao zote zinaburudisha, zinaelimisha na kufurahisha watu katika jamii. Mwimbaji mwenye nyimbo nyingi zaidi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Bebe Cool. Ana nyimbo zaidi ya mia moja (100).

Mwimbaji maarufu sana nchini Tanzania na ni Diamond Platinumz. Nyimbo zake zinavuma sana hapa Afrika Mashariki na duniani kote. Fundi mitambo wa Diamond Platinumz anaitwa Master Jay na anasema kwamba Diamond ana nyimbo zaidi ya 50.

Watu wengi wanaenda kwenye matamasha, Kilabu na diskoni usiku kwa sababu wanataka kusikiliza na kucheza muziki mzuri wa waimbaji hao. Vijana wa siku hizi wavulana kwa wasichana wanajua kucheza muziki vizuri. Wasichana wanatingisha matiti na matako yao pamoja na sehemu nyingine za mwili. Wavulana wanarukaruka juu na chini huku wakichanganya miguu yao. Lakini kati ya wavulana na wasichana ni nani wanaojua kucheza vizuri zaidi? Muziki ni mzuri kwa kila mtu hata wakiwa watoto wadogo, vijana, wakubwa na wazee. Kwa kweli,Watu wote wanapenda muziki duniani. Wazee wengi wanataka sana kusikiliza muziki wa zamani, yaani ule muziki wa enzi zao . Baadhi ya wazee wanapendelea sana muziki mwororo wenye mwendo wa polepole.

Ninaitwa Mukungu Collins. Mimi ni mvulana mwenye umri wa miaka kumi na Sita. Mimi ni

mwananchi wa Uganda. Ninaishi mjini Kawempe, kaskazini mwa jiji la kampala. Mimi kama kijana wa kizazi kipya ninapendealea zaidi mziki wa Kijamaica maishani mwangu. Kuna waimbaji wakubwa wa kijamaica kama vile; Konshens, Busy Signal, Nicki Minaj, Bennie Man, Mr.Vegas, Patra, Tiana, Shaggy, Alaine, Kartel na Gyptian. Ni kweli kwamba Wajamaica wanaimba vizuri muziki wao wa aina ya reggae , ragga na dance hall.

Lakini mimi kama mpenda mziki, ninaona kwamba Wimbo mzuri wa mwaka uliopita ulikuwa 'Kutama'*!* Wimbo huo umeimbwa na Fik Fameika. Mbali na wimbo huo, Mwanamziki huyo Fik Fameika ana nyimbo nyingine nyingi nzuri. Kwa mfano; Mbega wa baala, Gwe abisobola, Kachima, Mafia, Movie, Somebody, Mutuwulira, Property, Pistol , nakadhalika…

Hapa shuleni ninao Marafiki wengi sana ambao wanapenda mziki kama mimi. Wengi wao ninasoma nao Kiswahili katika kidato cha tatu. Miongoni mwa marafiki hawa ni; Twebaze, Agaba, Adinani, Bashir, Mutoni , Bukenya na katusiime . Tunapendana mno kama mlevi na pombe. Wanafunzi hao wanajua kuimba nyimbo na kucheza mziki wa kila aina. Tunacheza pamoja kwenye kikundi cha Nato katika Kilabu ya EAC. Wanajua kucheza Lingala, Hip-hop, B-Boy, Dance hall, RnB, nakadhalika..

***Maswali;..***

(a) Mwandishi wa habari hiyo ni nani? Je, ni mwananchi wa nchi gani?.

……………………………………………………………………………..

..........................................................................................

(b) Mwandishi ana umri wa miaka mingapi? Anasoma kidato cha ngapi?

………………………………………………………………………………….

..........................................................................................

(c) Mwandishi anapendelea zaidi muziki wa aina gani?

……………………………………………………………………………

(d) .Wazee wanapendelea sana kusikiliza na kucheza muziki wa aina gani?

…………………………………………………………………………………

(e) Mwandishi pamoja na familia yake wanaishi wapi?

…………………………………………………………………………………..

f) Andika majina ya waimbaji wakubwa sana Afrika mashariki.

1……………………… 2………………………… 3…………………….

4………………………… 5…………………….

g) NI nani Mwimbaji mkubwa wa mwaka elfu mbili kumi na saba? Aliimba wimbo gani?

……………………………………………………………………………………..

h) Toa umuhimu wa muziki kwa watu katika jamii.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

i) Wewe kama mtoto wa kizazi kipya, unataka kucheza muziki wa aina gani?

..........................................................................................

j) Andika majina manne ya wanamuziki wako wakubwa wa kijamaica.

1......................... 2......................... 3...................... 4...................

k) i) Ni mwimbaji gani maarufu anayevuma sana nchini Tanzania?

..................................................................................................

ii)Je, ana jumla ya nyimbo ngapi?

**2. Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata;**

*(Alama 20)*

Watoto ni muhimu sana katika jamii. Wao ndio watakaokuwa viongozi wa siku zijazo. Kwa mfano, wengine watakuwa maraisi, wabunge, madakatari, walimu, wahandisi na hata wauguzi. Inafaa wakuwa kaika mazingira yafaayo ili ndoto hii itimie. Mtoto vile vile anapaswa kufahamu wajibu wake katika kufanika maisha yake. Ni vizuri sote tuelewe na tuendeleze haki za watoto.

Kuna yale mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na makao. Jambo moja la kuzingatia ni lishe bora kwani humwezesha mtoto kukua akiwa na afya bora. Afya bora humsaidia mtoto kuepukana na maradhi ya aina nyingi na pia humsaidia kujimudu katika michezo na shughuli za kusoma.

Kila mtoto anahitaji makao maalum anakoweza kuita nyumbani. Mahali ambapo anaweza kuishi kwa usalama na kuhisi mapenzi ya wazazi na jamaa zake. Ukosefu wa makoa Unaweza Kusababisha mtoto kukimbilia mitaani na kurandaranda ovyoovyo. Akiwa huko mitaani hukumbwa na matatizo mengi kama vile ukosefu wa chakula, utumiaji wa dawa za kulevya, uasherati, kutungwa mimba na ndoa za mapema

Mtoto anatakiwa kuhakikisha usalama wake kwa kuelimishwa hadi kiwango cha juu iwezikanavyo. Kila mtoto anashauriwa kufanya bidii masomoni mwake iwapo anataka maisha mazuri baadaye. Inafaa Mtoto azingatie maadili ya Wazazi wake ili aweze kufua dafu maishani. Kwani asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Mtoto mwerevu ni Yule atakayeweza kuchuja Mila za jamii yake na kuamua kati ya zinazofaa na zile zisizofaa. Kwa mfano, kuhusu tohara za watoto wa kike na pia Wasichana wachanga kuozwa kwa Wazee. Endapo Wavulana watapashwa tohara, basi ifanyike katika vituo vya afya au katika mazingira safi

Yafaa mtoto aelewe na akuwe katika mazingira yenye amani. Aishi katika jamii akihisi Mapenzi na hali ya Usalama. Hili litamwezesha kuishi akijiamini na kujithamini, na hivyo ataweza kuwapenda hata Majirani zake na kuwajalia Maslahi.

**Maswali:**

(a) Pendekeza Kichwa Mwafaka cha hadithi hii (alama 02)

(b) Andika mahitaji matatu ya kimsingi kama yanavyopatikana katika kifungu hiki. (alama 02)

(c) Taja Umuhimu wa kuwatunza Watoto. (alama 02)

(d) Mtoto anahitaji kufanya nini kuhusu Elimu? (alama 02)

(e) Eleza matatizo Manne yanayoweza kumkumba mtoto huko Mitaani. (alama 02)

(f) Je, kupashwa tohara kwa Wasichana ni vizuri au la? Toa maoni yako? (alama 02)

(g) Eleza maana ya Methali, “Asiyesikia la mkuu huvunjika guu” (alama 02)

(h) Katika jamii yako, ni Mila gani ambazo zimepitwa na wakati? Toa sababu zako. (alama 02)

(i) Hadithi hii inakufunza nini wewe kama Mwanafunzi? (alama 02)

(j) Eleza maana ya maneno haya kutokana na taarifa hii ya habari;

(i) Maadili (alama 01)

(ii) Wahandisi (alama 01)

**1. Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini.**

Ivy ni mwananchi wa Uganda. Ni mschana mwenye umri wa miaka kumi na sita. Anaishi katika wilaya ya Nakaseke pamoja na wazazi wake.Wazazi wa msichana huyu ni wafanyabiashara na wanapata pesa nyingi kutokana na kazi yao hiyo. Wana maduka Matatu hapa jijini kampala. Wanauza bidhaa kama vile; viatu na Nguo za wanaume na wanawake, mikoba katika duka lao la kwanza , Viatu vya wanawake na wanaume –wadogo na wakubwa. Kwenye duka lingine wanauza simu na vyombo mbalimbali vya simu, Duka lao la tatu ni la kompyuta na vifaa vyake nakadhalika. Pesa takribani zote wanazozipata wanazilipa shuleni kama karo ili binti yao Ivy asome.

Huyu mtoto wa kike Ivy ndiye kifungua mimba katika familia ya Bwana Mukiri na Bi. Nakazzi. wazazi wote wawili, yaani baba na mama yake wanampenda sana mtoto wao si kwa sababu ya kuwa wa kwanza kuzaliwa katika familia yao tu, bali pia ni kwa sababu ni mwerevu sana masomoni. Kila muhula na kila mwaka, yeye ndiye anachukua nafasi ya kwanza na kuwaongoza wengine darasani.Ivy ni mwanafunzi katika shule ya upili ya Nakaseeta na anasomea katika kidato cha tatu.

Mwaka uliopita, aliwashinda wanafunzi wote wa kidato cha pili. Waswahili walisema kweli kwamba akili ni mali na hawakukosea kwa sababu Ivy alipewa zawadi chungu nzima kutoka kwa mkurugenzi wa shule,walimu, wazazi na marafiki zake. Lakini zawadi ambayo kwa kweli ilikuwa kubwa sana kuliko zote alizozipata siku hiyo ni udhamini. Ivy alipewa nafasi ya kusomea bure mpaka atakapomalizia masomo yake ya sekondari katika shule yake hiyo ya Nakaseeta. Shule ya Ivy iliamua kuchukua jukumu la kumdhamini na kugharamia masomo yake baada ya kuona na kuhakikisha kwamba msichana huyu anapenda sana kusoma na ni mwenye bidii masomoni. Isitoshe, kila kitu anachokifanya, anakifanya kwa nguvu na moyo mmoja. kwa mfano; kucheza michezo kiwanjani, kuimba kwenye kwaya ya shule na kulima shambani. Baba na mamake Ivy, yaani Mzee Mukiri na Bi.Nakazzi wote wanasema kwamba mtoto wao Ivy amekuwa mwerevu sana tangu utotoni mpaka sasa ukubwani hajabadilika hata kidogo.

Walimu wote ambao waliwahi kumfundisha Ivy darasani, wanasema kwamba ndiye mwanafunzi pekee anayeweza kukwangula alama takribani zote, na wakati mwingine hupata asilimia mia moja katika mitihani na mazoezi. Mwalimu wake wa somo la Kiswahili bwana Kisitu Samuel naye anasema ,"Ivy ni mwanafunzi mwerevu na hodari masomoni na anapendelea sana somo la lugha ya Kiswahili"

***Maswali;***

a. Ivy ni mwananchi wa nchi gani?

………………………........................................……………

b. Wazazi wake Ivy wanaishi katika wilaya gani?

………………………………..........................................………

c. Andika machache Kuhusu wazazi wa Ivy.

..........................................……………………………………………

d. Kwa nini walimu na walimu walimpenda sana Ivy ?

...........................................................................................................

e. Wazazi wake Ivy wanafanya kazi gani?

......................................................................................................

…………………………………………………………………………………

f. Ivy anasomea katika shule gani? Na anasoma katika kadato cha ngapi?

...............................................................................................................

g. Toa sababu kwanini shule ya Ivy inadhamini masomo yake?

……………………………..........................................................................

……………………………………………………………………………

h. Taja mambo mawili mazuri ambayo Ivy anayafanya.

.....................................................................................................

………………………………………………………………………………………

i. Pendekeza mada mwafaka kwa habari hiyo.

………………………………………………………………………………………

j. Kwa nini wazazi na walimu wa Ivy wanampenda sana?

.....................................................................................................

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;.**

Karibu na kijiji maarufu cha Nimirokukabala- wilayani Nakaseke, paliishi mwanamume mmoja aliyejulikana kwa jina Bwana Mudiribada Zephaniah. Na mke wake alikuwa akiitwa Bibi Musama Suzana. Familia hii haikuwa maskini wala tajiri.Ilikuwa ya wastani kiuchumi. Hata hivyo, walikuwa hawaazimwi nguo, hawaombi sukari wala chumvi kwa majirani yao. katika familia hii kulikuwa na watoto kumi . wasichana wakiwa watatu na wavulana saba. Kifungua mimba yaani mtoto wa kwanza kuzaliwa katika familia hii alikuwa ni msichana ilhali kitinda mimba ni mvulana. Watoto hawa walikua vizuri wakiwa wazima wa afya.

Bwana Mudiribada alikuwa mkulima maarufu sana. Mwaka wa 1995, Mudiribada ndiye aliyeshinda wakulima wote katika wilaya nzima ya Nakaseke. Shamba lake kubwa lilikuwa limejaa mimea ya aina mbalimbali na mifugo. Alikuwa na wafanyakazi chungu nzima ambao walimsaidia sana katika kazi nyingi pale shambani. Familia nzima; yaani baba, mama na watoto walikuwa wakiamka asubuhi na mapema kwenda kufanya kazi za shambani kila siku, isipokuwa Jumapili tu. Siku ya Jumapili ilikuwa siku ya kuenda kuhudhuria maombi kanisani.Watu takribani wote katika familia hii walikuwa wachamungu. Kwa hivyo, kwa mtu mchamungu ni vigumu sana kukosa maombi kanisani siku ya Jumapili. Watoto watatu walikuwa waimbaji katika kwaya ya kanisa.

Kuna shughuli nyingi sana ambazo Bw.Mudiribada alihakikisha kwamba zinafanywa ndani ya wakati ili shamba lake liweze kulete faida kubwa. Kazi ya kwanza ni kufyeka na kulima konde au shamba. Magugu yanalimwa na kung’olewa, nyasi zinakusanywa na kuchomwa moto. Kazi ya pili ni kupanda. Kupanda ni kitendo cha kuweka mbegu ardhini ili ziote. Baada ya siku chache, mbegu zinaanza kuota kutoka ardhini. Kazi ya tatu ni kupalilia. Kupalilia ni kitendo cha kulima na kung’oa magugu na nyasi ili mimea iweze kukua vizuri, kuchanua vizuri na kuzaa matunda na chakula. Kazi ya nne ni kumwagilia. Umwagiliaji ni kitendo cha kunyunyuzia mimea maji ili mimea hiyo iwe na maji ya kutosha ya kuiwezesha kukua vizuri.

Pia kuna kazi ya tano ya kunyunyuzia dawa na mbelea kwenye mimea. kazi ya kunyunyuzia mbolea pamoja na dawa ya kupiga vita wadudu na ugonjwa wa mimea. Mimea yenye kinga ya dawa na mbolea inakua vizuri na kunawiri. Kazi ya sita ni kuvuna. Baada ya matunda au chakula kwenye mimea kukomaa vizuri, wafanyakazi wanavuna chakula ama matunda au mazao hayo na kuyatoa shambani. Kila baada ya mazao kuvunwa shambani, mazao kama vile; mahindi, maharagwe, mtama na wimbi; yalikuwa yakipelekwa nyumbani na kuwekwa au kuhifadhiwa kwenye ghala. Mazao mengine kama vile; matunda na mboga yalikuwa yakipelekwa sokoni kuuzwa kabla ya kuharibika.

Mazao mengine kama vile; Pamba, kahawa, ngano na mchele; yanaweza kuchukuliwa kuuzwa viwandani kama malighafi baada ya kuyakausha vizuri ili kutengenezea chakula, bidhaa na vifaa mbalimbali.

Kwa hivyo, Bw.Mudiribada alikuwa anaingiza pesa nyingi baada ya kuuza mazao yake sokoni.Pia alikuwa anapata chakula cha kutosha kulisha familia yake nzima.

***Maswali;***

a) kulingana na habari, ni nani mkuu wa familia katika hadithi?

b) Kifungua na kifunga mimba wa Bw.Mudiribada walikuwa watoto gani?

c) Eleza kazi sita ambazo Bw.Mudiribada alihakikisha kwamba zinafanywa vizuri ndani ya wakati ufaao hapo kwenye shamba lake.

d) Bw.Mudiribada hakuwa mtu maskini wala tajiri sana. Unadhani ni kwa sababu gani?

e) Familia ya mwandishi ilikuwa inapatikana wapi nchini Uganda?

f) Umaarufu wa Bw.Mudiribada Zephaniah ulitokana na kazi gani haswa?

g) Bw.Mudiribada alipata mafanikio gani katika mwaka wa 1995?

h) Pendekeza mada au kichwa cha habari kilicho mwafaka kwa habari hiyo.

i) Kwa nini mwandishi wa habari anasema kwamba familia ya Bw.Mudiribada ilikuwa ya watu Wachamungu? Toa sababu mbili.

j) Baada ya Bwana Mudiribada kuvuna mazao yake shambani, mazao hayo yalikuwa yakichukuliwa sehemu mbalimbali. Andika majina ya mazao;-

   i. Yaliyohifadhiwa kwenye ghala;
   ii. Yaliyokuwa yakipelekwa sokoni;
   iii. Yaliyokuwa yakipelekwa viwandani kama malighafi ya kutengenezea bidhaa;

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;.**

**JUHUDI**

Baada ya vuta nikuvute za ulezi wa mimba na patashika ya kite cha mzazi, Juhudi alizaliwa salama salimini. Huko nje Mzee Sulubu alikuwa hajijui wala hajitambui kwa sababu ya wasiwasi uliompata. Alitangatanga huku na kule namna ya koo aliyetaka kubwaga yai. Alipopashwa habari kuwa kiumbe mpya amewasili ulimwenguni alibubujikwa na machozi ya furaha. Jambo lililomfurahisha Sulubu ni kuwa mkewe Samaha kapata salama.

Mzee Sulubu alikuwa maskini hohehahe. Jambo hili lilimpelekea Juhudi kulelewa katika hali ya ukata. Ingawa mkata hapati mwana, Sulubu alikwenda juu chini ili aweze kumlea mwanawe wa pekee. Juhudi alipofikia umri wa kwenda shule, alipelekwa shuleni na kuendelea na masomo yake ya msingi hadi akamaliza. Aliendelea vizuri masomoni lakini kwa bahati mbaya wazazi wake wote wawili waliaga dunia punde tu baada ya mtihani wake wa darasa la nane. Matokeo yalipotangazwa alizidi kutumbukia katika lindi la ukiwa ingawa alifaulu vizuri. Alijiuliza ni kwa nini wazazi wake walimwacha wakati ule. Pia alijiuliza ni kwa nini wawe wao. Hatimaye aliamua kumuepusha ibilisi na kumshukuru Mungu.

Juhudi aliwashukuru wazazi wake na kuwaombea Jalia awaweke mahali pema peponi. Ingawa alikutana na mitihani mingi ya kimaisha aliweza kufaulu maridhawa. Bila kupoteza wakati aliamua kuingia katika kazi ya uvuvi huku akingojea kujiunga na kidato cha kwanza. Kutokana na juhudi alizokuwa nazo na kwa uwezo wa Karima alipata pesa za kumwezesha kujiunga na shule ya upili. Juhudi hakuwa na budi ila kuzipania nguo zake na kutia juhudi masomoni. Aliendelea na kujilipia karo hadi akamaliza kidato cha nne. Katika kipindi hicho hakuna hata mtu mmoja liyejitokeza kumsaidia. Si kuwa hakuwa na ami waliojiweza. La! Walikuweko tele waliokuwa na mali kochokocho, lakini maskini hana ndugu. Hata hivyo, mja akifunga wake wa Maulana u wazi.

Matokeo ya mitihani ya shule za upili yalipotangazwa Juhudi aliibuka wa kwanza katika nchini nzima. Jambo hili lilimpatia udhamini wa serikali katika masomo yake ya juu. Bila ya kusita alichagua kuwa nahodha wameli. Alifanya hivyo kutokana na vile kazi ya uvuvi ilivyomsaidia masomoni. Jambo hilo lilimfanya aheshimu sana hahari. Serikali ilimpeleka Ureno ili asomeee kazi hiyo. Naye baada ya miaka saba alihitimu. Baada ya mahafali alitunukiwa shahada ya unahodhawa meli. Juhudi aliajiriwa na kampuni kubwa ya meli na kuanza kuuzuru ulimwengu. Alitembelea nchi nyingi za Afrika kama vile Afrika Kusini, Unguja, Tanzania, Msumbiji, Ushelisheli na kadhalika. Nchi za ulaya alizotembelea zilikuwa Ufaransa, Uingereza, Ujerumani na nyingine nyingi. Ajipokawa akirudi nyumbani, wale waliomuepuka kama mgonjwa wa ukoma walimpiga makamama. Ami zake waliompa kisogo wakati ule wa giza walimpokea kwa shangwe nanderemo. Ingawa anyolewaye kwa chupa hasahau, Juhudi aliyapurukusha madhila yote waliyomtendea na kuwaheshimu vilivyo. Walipoona hivyo majuto yaliwajia lakini ifaliye nini nayo maji yakimwagika huwa hayazoleki? Walibaki kumpiga makumatio na kujimamia ovyo ovyo. Juhudi aliwasamehe na kuwaambia kuwa yaliyopita si ndwele wagange yajayo.

**Jibu maswali haya:**

1. Ni jambo gani lililomfanya Sulubu kutangatanga kama kuku aliyetaka kutega yai?
2. Kwa nini Sulubu alitokwa na machozi?
3. Samaha alizaa mtoto wa kike au wa kiume?
4. Ni nini maana ya: <u>Alizidi kutumbukia katika lindi la ukiwa?</u>
5. Taja mitihani ya kimaisha aliyokutana nayo Juhudi.
6. Ni nani aliyemlipia Juhudi karo katika shule ya upili?
7. Je, Juhudi alikwa na jamaa zake wengine? Eleza.

8. Kwanini Juhudi aliamua kusomea unahodha wa meli?

9. Ambatanisha jina la Juhudi na matukio katika habari hii.

10. Eleza maana ya:

(a) Walimpa kisogo

(b) Ukoma

***2. Soma taarifa ya habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini yake:***

Kiswahili ni Lugha ya Kiafrika iliyotokea kutokana na mwingiliano wa maneno hususa ya Kibantu na Kiarabu. Kiswahili ni Kibantu na siyo Kiarabu kama watu wengine wasemavyo. Asili ya Kiswahili inaaminika kuwa pwani ya Afrika Mashariki. Hapa ndipo waarabu kutoka Uarabuni waliposhirikiana na waafrika katika shughuli mbalimbali .Na katika shughuli zao walikuwa wanachanganya maneno ya kibantu na kiarabu ili waweze kuwasiliana na kuelewana vizuri. Matokeo yake yakaunda lugha mpya ya mseto. Lugha hiyo mpya ikaja kujulikana kama - Kiswahili.

Kuna sababu nyingi zilizosaidia Kiswahili kuenea na kusambaa kwa mwendo wa kasi duniani; Biashara, Dini, Ndoa kati ya waarabu na waafrika, Ukoloni, Afrika kupata Uhuru , vyombo vya habari, Elimu, siasa za kizalendo, uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili, ukuaji wa teknolojia,Uhamaji na uhamiaji, utendawazi.

Kiswahili ni lugha ya kibantu na hii kwa sababu asilimia kubwa kwa takriban asilimia sabini na tano ya maneno yanayotumika katika Kiswahili yanapatikana kwenye lugha nyingi za kibantu.

Miaka ya karne ya kumi, mataifa ya mbali yalijaribu kuja Afrika ya Mashariki, hasa mataifa ya mashariki ya mbali kama Waarabu, waajemi, Wahindi na hata Wachina. Kilichowaleta kilikuwa zaidi ni biashara. Kwa sababu labda ya umbali, mataifa yayo hayo hayakuja kwa wingi kama Waarabu. Waarabu waliishi karibu na Afrika na walizidi kupapenda Afrika Mashariki kwa ajili ya biashara ya Watumwa, pembe za ndovu na isitoshe dini ya Kiislamu ilipoanzishwa huko Uarabuni, walitaka kuieneza mbali. Waarabu wengine walikuja pande hizi ili kuieneza dini hiyo na walipata wafuasi wengi.

Wavumbuzi kama Livingstone, Speke, Grant, Burton, kina Baker na Henry Murton Starnly, walipofika sehemu hizi za Afrika, watu wa Ulayawalizidi kuvutiwa na Bara la Afrika hasa Afrika Mashariki.

Mashirika ya dini huko Ulaya yalitaka Waafrika wafunzwe dini na kukomesha biashara ya watumwa. Walitaka kujua zaidi juu ya Afrika Mashariki. Wamisheni na wavumbuzi Krapf na Rebmann, walitumwa na shirika la dini lililoitwa ‘The Church Missionary Society’ huko Rabai Pwani. Wajerumani nao waliendesha mambo ya dini ya kuanza kukomesha biashara ya watumwa. Maenezi ya dini yaliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili. Askofu Edward Steere alianzisha maandishi kwa Kiswahili. Jinsi shughuli za kidini zilivyoendelea kutumia Kiswahili na jinsi maandishi kwa lugha ya Kiswahili yalivyozidi, ndivyo Kiswahili kilivyoendelea kusambaa na kuenea vururu dunan. Kamusi ya kwanza ya Kiswahili iliandikwa na Daktari Ludwig Krapf.

Waarabu nao kufikia miaka ya karne ya kumi na tisa, walikuwa wamepenya mbali, wengi wakiwa wamefika hadi Kongo na Uganda. Wengine walishika hatamu uongozini, hasa sehemu za Zanzibar.

Kiswahili kilizidi kutumika hasa katika miji na zile sehemu zilizokuwa njia kuu za kusafirishia watumwa.

Watawala hawa walijaribu kukitumia Kiswahili na kukiruhusu kitumike katika shughuli za utawala, dini na kazi mashambani. Maandishi yalizidi kuandikwa kupitia magazetini, vitabuni na shule zilianzishwa na wanafunzi walifunzwa Kiswahili. Miji ilikua na watu walizidi kukutana na kutumia Kiswahili. Lakini mnyonge kupata ni mwenye nguvu kupenda. Kama hawa watawala wangekikataza Kiswahili pengine kisingepiga hatua kubwa.

Mgala muue na haki umpe. Ingawa wazungu wengine walikuwa wakatili, kulikuwa na wengine waliokipenda kiswahili na kukiendeleza hata kimaandishi. Ilipofikia mwaka wa 1925, Gavana wa Tanganyika, Muingereza, aliiona haja ya kuisanifisha lugha. Aliitisha mkutano wa Afrika Mashariki na kutaka kuanzishwe baraza la Kiswahili la kusanifisha lugha.

Kiswahili kilisanifishwa sana kuunganisha watu na kilitumika sana shuleni, mijini, redioni, magazetini, kwenye sahani za santuri, katika michezo ya kuigiza, vitabuni, televisheni na hata sasa kinazidi kutia fora kwani kimefanywa somo la lazima na kinazungumzwa na mamilioni ya watu duniani hasa Afrika Mashariki.

**MASWALI:**

a) Pendekeza mada mwafaka kwa taarifa ya habari hiyo. (alama 02)

b) Ni ni maana ya Kiswahili? *(Alama 03)*

c) Kwa nini Waarabu walikopesha lugha ya Kiswahili maneno mengi kuliko mataifa mengine? *(Alama 03)*

d) Kwa nini mwandishi amesema, ‘Mnyonge kupata ni mwenye nguvu kupenda’? *(Alama 02)*

e) Ni mataifa gani ambayo yaliingiliana na Waafrika wa Afrika Mashariki kabla ya karne ya ishirini? *(Alama 02)*

*f)* Wavumbuzi na wamisheni walisaidiaje katika ukuaji wa Kiswahili? *(Alama 04)*

g) Ni sababu gani zilizofanya mataifa mengine yapende kuja Afrika Mashariki? *(Alama 04)*

h) Ni sababu gani zilizoimarisha maenezi ya Kiswahili? Fafanua sababu nne. (*Alama 04*)

i) Andika methali yoyote moja iliyotumiwa katika habari hiyo. *(Alama 02)*

j) Waafrika walifaidikaje kutokana na wageni walioingia bara la Afrika kabla na baada ya karne ya ishirini? (Alama 5)

k) Hawa ni watu gani katika habari hiyo? *(Alama 03)*

I) Wamisheni

II) Wavumbuzi

III) Wakoloni

ZOEZI LA KWANZA

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yaliyoulizwa.

Dawa takriban za aina zote huathiri miili yetu inavyofanya kazi, hivyo hatuna budi tuzitumie kwa uangalifu. Matumizi mabaya ya dawa husababisha athari mbaya kwa mtumiaji. Aghalabu matumizi ya dawa husababsha matatizo shuleni , nyumbani na kwingineko kwani mtumiaji anaweza kuvunja sheria za jamii na za nchi.

Aidha dawa haramu kama vile bangi, kokeini na heroini ni hatari zaidi kwani hutumiwa vibaya bila kuzingatia ushauri wa kitaalamu na hivyo kusababisha athari zaidi na hata kuleta maambukizi ya magonjwa kama ukimwi.

Matumizi ya dawa yanaweza kuwa ya muda mfupi au mrefu na athari zake hutokea kwa watumiaji wote. Baadhi ya watu hutumia dawa maisha yao yote, hususan wenye magonjwa ya muda mrefu kama kifafa, kisukari, mtindio wa ubongo na kadhalika.

Matumizi mabaya ya dawa ni yale yasiyolenga kuboresha afya ya mtu iwe kwa makusudi au kwa kutoelewa taratibu za utumiaji na hivyo kuleta madhara makubwa kwa mtumiaji. Mathalani mtu anatumia dawa bila kushauriwa na wataalamu au anagawa dawa zake kwa mgonjwa mwingine bila kufuata vipimo vya kitaalamu.

Pombe ni kinywaji ambacho kama kikitumiwa vibaya athari kubwa kama iivyo katika matumizi mabaya ya dawa. Mathalani mtu aliyelewa kupita kiasi hushindwa kujimudu na na hivyo huweza kusababisha vurugu, ajali sambamba na mtumiaji wa dawa kama bangi, kokeini na heroini.

Dawa , siku zote ni nzuri kama zitatumika kwa malengo mazuri na kufuata vipimo na ushauri wa wataalamu. Wataalamu hawana budi kuwaelimisha watumiaji faida na hasara za kila dawa wanayotumia, vinginevyo dawa tunazotumia vyingi ni muhali kwa afya zetu. Suala la msingi la kuzingatia ni kwamba dawa hazipo kwa ajili ya kuburudisha watu bali kwa matibabu ya watu. Hivyo, tuwe makini kwa hili kwani mzaha mwisho ni usaha.

2.Soma habari ifuatayo kwa makini kisha uifupishe kwa maneno 50.

Mtindo wa urasmi ni ue wa kuipasha hadhira habari maalum. Sifa mojawapo ya mtindo huu ni ile ya kutoa taarifa fupi muhimu na zile ambazo zimeeleweka. Aidha uteuzi wa maneno ambayo yanafahamika au yanaweza kufahamika kwa urahisi.

Tunaposema kutoa taarifa fupi tuna maana ya sentensi au kauli fupi hizi zinaweza kumfikia msikilizaji na kutuama akilini kwa urahisi zaidi kuliko sentensi ndefu. Ni muhimu

kwa vile taarifa rasmi hubeba ujumbe maalum ambao inapasa uzingatiwe. Ni kwa mantiki hiyo ambapo matumizi ya sentensi zinazoeleweka yanakuwa muhimu sana hapa. Taarifa rasmi huwa kwa kiasi Fulani kavu, yaani haina madoido, ingawa ipo nafasi ya kucheza na sauti.

Katika matumizi ya maneno yanayoeleweka umuhimu wake umekitwa kwenye lengo hilo hilo la kuufikisha ujumbe katika hali ya kueleweka kikamilifu.

3.Soma taarifa ifuatayo kwa makini kisha uitafsiri katika lugha ya Kiingereza.

The Ozo men were now to choose a new chief and oat first it seemed they in for an easy task. It wouldn't be like the last section when so many bad words had passed between Ikoo and uwadiegwu and so much bad medicine had been thrown about for the purpose of influencing the minds of opponents. On that occasion there had been problems of *procedure* to be settled and about this there had been as many opinions as there were Ozos or even commoners in Aniocha. This time the steps to be followed were plain. Seven *market weeks* after the death of the last chief, candidates to fill the vacancy were to be called for from all the families. The Ozos would meet and, voting secretly, select the most suitable.

There was little doubt who it would be. Araba. His father had ruled before Idemmili. He had many other qualifications: a long barn, ten women, a house of which *much noise was made*. Araba was known too to have always been a fighter for Aniocha and the Awadiegwus. Finally and most important of all, he had taken the Ozo title before anybody alive. No one could have stronger claims to the chieftaincy. There were people, though, who had doubts about Araba's qualities as a ruler. They feared his arrogance and his fondness for *litigation*. He had taken many people to the village court and had in most cases triumphed. Manu people called him 'that big head', referring both *literally* to the size of his head and *metaphorically* to the size of his pride. So it seemed to that if he became chief he would be *open-handed*. One was always sure of a cup of palm-wine in Araba's compound – and honest- 'Araba *hasn't two mouths*,' people said, 'when he says yes it is yes' – but he would also be stern and obstinate and always quarrelling with Ozos.

(Adopted from *Practice English* 3, Ogundipe)

4. Soma habari ifuatayo kisha uifupishe kwa maneno 100.

Viazi ni aina ya vyakula vya mizizi. Kimoja ni kiazi. Kuna aina nyingi za viazi. Kwanza ni viazi vitamu. Hivi hulimwa sana katika nchi za joto kama hizi zetu za Afrika ya Mashariki. Viazi vyenyewe ni vitamu vivyo hivyo jinsi vinavyoitwa.

Viazi vitamu huliwa kwa kupikwa au kuchomwa. Pia huweza kugegedwa ama kutafunwa bila kupikwa. Upishi hasa wa viazi ni kutkoswa. Yaani hutiwa chunguni au sufuriani kisha hutiwa maji kiasi cha kutosha. Huchemshwa kwa muda hadi viazi vyote view vimelainika kama samli. Chungu huepuliwa kisha viazi hupakuliwa na kutiwa kinywani baada ya kupulizwa na upepo. Viazi hivyo huweza kuliwa kwa kitoweo chochote kama vile nyama ,

samaki, mboga au mchuzi. Pia huwa kitafunio kizuri sana cha kinywaji kama chai, uji au maziwa.

Aina nyingine za viazi ni yugwa au jimbi. Pia huitwa kiazi kikuu. Hupikwa kwa kutokoswa kwenye maji au mafuta lakini huwezi kukigegeda kikiwa kibichi.

Viazi vingine ni mbatata. Wengine huviita viazi viviringo au viazi ulaya. Hivi havina ladha yoyote tamu, lakini vinaliwa sana. Tena kwa namna nyingi mno. Huunga supu vizuri sana. Hutokoswa kwa kutiwa chumvi na mafuta na kuwa kitoweo. Aidha hukatwa vipande bapa kama silesi ya mkate na kutengenezwa kaukau. Kwa kimombo kaukau hizo huitwa *krispi*. Mapishi mengine ya mapata ni kukatwakatwa mifano ya vijidole na kukaangwa kwenye mafuta mengi. Baada ya kuiva hutolewa kutoka katika mafuta hayo na kupakuliwa kwenye vijisahani ambapo baada ya kurashiarashia chumvi, nyanya au achari, huwa chakula kitamu kupindukia. Hicho ndicho chakula maarufu cha walaji wa siku hizi mjini. Na endapo wewe pia umezoea Kimombo kama wenzako, ukiite *chipsi*.

Karoti ni aina nyingine ya kiazi. Zenyewe hutumika hasa kama kiungo hasa kama kiungo cha kachumbari, mchuzi ama huliwa mbichi.

Viazi vitamu vinaweza kupandwa kwenye vichuguu, matuta au kwa njia ya kawaida ya kilimo cha sesa. Yugwa hulimwa mahali popote mradi pawe na mvua ya kutosha. Viazi vitamu ni chakula cha kuongeza nguvu mwilini kutokana na ungaunga wake. Majini ya viazi vitamu huitwa marando au marau kama vie majani ya muhgo yanvyoitwa kisamvu.

5. Zamani palikuwepo mtoto mmoja aliyeitwa Rambaramba. Mtoto huyu wa kiume alitoka kwa familia moja tajiri na walikuwa wanaishi katika kijiji au mtaa wa Shime. Babake aliitwa Amani na kweli mwanamume huyu alikuwa mwenye heshima na upendo kwa wakubwa na wadogo.

Rambaramba alikuwa mtoto mtundu au mtukutu sana alipokuwa na umri wa miaka mitano, alijulikana sana mtaani kote kwa matendo yake maovu au mabaya sana. Watoto wote wa rika lake hawakuthubutu kucheza naye. Kila walipojaribu, aliwagota au kuwasukuma sukuma, kuwapiga teke na kuwabwaga chini. Watoto wote walimwogopa na kumhepa. Watoto wengi walikataa kucheza naye. Hiyo nayo haikuwa dawa, aliwafuata na kuwapiga mawe. Ijapo babake, yaani Mzee Amani alimkanya mara kwa mara, mtoto huyu hakusikiliza maneno hayo na akandelea na tabia yake mbaya.

Alipokuwa na umri wa miaka saba, Rambaramba alipelekwa shule ya msingi karibu na kwao ambapo tabia yake haikubadilika sana. Lakini alipofika darasa la sita mambo yalichacha. Siku moja Rambaramba alimpiga mwanafunzi mwenzake kwa jiwe karibu kumtoa jicho. Habari hizi zilipomfikia Mzee Amani mara moja naye alikwenda haraka haraka hapo shuleni. Huko alipata kwamba yule mtoto aliyeumizwa amepelekwa hospitali kwa matibabu.

Kwa masikitiko Mzee Amani alikubaliana na walimu kwamba mwanawe apewe adhabu na ushauri. Basi Rambaramba alipewa adhabu ya kufyeka nyasi sehemu kubwa ya kiwanja cha kandanda.

Mwanzoni hakutaka kufyeka mahali hapo na ikawa lazima asimamiwe na mwalimu wake wa darasa ili afyeke. Baada ya kijana huyu kumaliza adhabu hiyo malengelenge yenye uchungu yalimtoa mikononi. Vidole vyake vilikuwa vimevimba na kumuuma sana.

Baada ya adhabu hii Rambaramba alianza kubadilisha tabia yake. Huku kubadilika kwa tabia yake kuliwafurahisha watu wote wakiwemo wazazi, wana-Kijiji na walimu wake. Pia, wanafunzi wenzake walianza kushirikiana naye katika michezo na shughuli nyinginezo.

Alipomaliza masomo yake ya shule ya msingi alifanywa kiongozi wa wanafunzi wenzake. Alifanya kazi hii vizuri sana hata alipewa zawadi ya mwanafunzi mwenye tabia nzuri. Nyumbani kwao aliwasaidia wazazi wake katika shughuli zote za nyumbani. Katika mitihani yake ya mwisho, alifaulu vizuri mitihani yake na akaendelea na masomo yake ya sekondari mpaka chuo kikuu.

Maswali

a) Kwa nini Mzee Amani alipendwa na watu wa kijiji chake?
b) Rambaramba alianza kuonyesha ishara za kuwa mtukutu akiwa na umri gani?
c) Kwa nini rika zake Rambaramba waliogopa kucheza naye?
d) Taja sababu za Rambaramba kupewa ushauri wa adhabu kali hapo shuleni.
e) Rambaramba alipewa adhabu gani baada ya kumpiga jiwe mwanafunzi mwenzake?
f) Mbona mwaimu alimsimamia Rambaramba afyeke nyasi kiwanjani?
g) Eleza kilichosababisha malengelenge yenye uchungu mikononi mwa kijana huyo.
h) Rambaramba Kubadili tabia yake kulimsaidiaje?
i) Ni akina nani waliofurahia mabadiliko mazuri ya tabia ya Rambaramba?
j) Andika mafunzo mawili unayopata katika hadithi hii.
k) Pendekeza kichwa cha habari kizuri kwa habari hii.

5. AKUFAAYE, MFAE

Katika msitu mmoja mkubwa kuliishi wanyama wengi, miongoni mwao wakiwa mbogo na buibui. Siku moja mwitu huo ulishika moto. Wanyama wote walishikwa na wasiwasi , wakaanza kukimbia ili wajiokoe. Mbogo alipokuwa akikimbia alikutana na Buibui aliyekuwa amejawa na hofu nyingi kwa sababu moto uliongezeka. Buibui akamwambia Mbogo, ‘Tafadhali Bwana Mbogo nichukue juu ya pembe zako ili nisiteketee motoni nami nitakusaidia

6. Tafsiri kwa Kiswahili habari ifuatayo.

The cassava plant is widely grown in tropical countries. It is a staple food depended upon by over 200,000,000 people. Its cultivation in more than 80 countries makes it the eighth most important food crop in the world.

The cassava or manioc, as it is known in French speaking Africa, is a drought resistant plant. There are also not many serious pests to the plant and varieties that are resistant to pests can always be grown. The cassava has advantages over other crops in that it can withstand adverse soil and weather conditions. The plant is grown at altitudes ranging from sea level to about 1600m.

The main edible part of the plant is the tuber though the green leaves can also be used a vegetable. The cassava plant forms tubers after four months of planting and is ready for lifting after twelve or eighteen months. There are other varieties of cassava which mature in seven to eight months of planting.

In east Africa, the plant grows fairly well and it is high time more research was done, particularly in the drought stricken areas. The tuber can be dried and used as food for human beings and farm animals. The cassava can also be turned into starch for use in textile and food manufacturing industries.

(East African Examinations Council)

7. Fupisha habari ifuatayo kwa maneno yasiyozidi 110.

Mtoto anapozaliwa huwa hana ujuzi wa dunia wala elimu ya aia yoyote ile. Mtoto a kishazaliwa ndipo anaaanza kukusanya ujuzi wa mambo ambayo humnufaisha katika kuishi kwake na huendelea kufanya hivyo hadi anapofikia kikomo cha maisha yake, yaani anapokufa. Katika kujifunza kwake, mtoto anatumia njia mbili za kujipatia mafunzo. Aina ya kwanza ni ile ambayo mtoto hujifunza mambo bila ya kujielewa kama anapata ujuzi, yaani hujifunza maarifa mapay moja kwa moja bila ya kuwa na nia maalum ya kutaka kujifunza. Tuseme kwa mfano, mtu anasikia mlio usio wa kawaida nje ya nyumba yake. Akigutuka, huwa ameshawishika na hamu ya udadisi wa kufanya hivyo

8. Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yaliyoulizwa.

Pasta wa kanisa moja katika kijiji hiki, alijipata pabaya **alipotwangwa** na mama alipompata akiongea na binti yake. Pasta huyo, anatambuliwa eneo hili kwa **ujasiri** wake wa **kueneza** injili na kufukuza **mapepo**. Hata hivyo, penyewe mtaani zasema kwamba baadhi ya watu hushuku kwamba ana tabia ya **kuwatongoza vipusa** lakini hakuna aliyewahi kumpata peupe akifanya hivyo.

Siku ya **kisanga** mwanadada aliyejaliwa sura ya **kuvutia** alimwendea pasta kuwasilisha ombi la kutaka kanisa limsaidie kulipa karo. Hata hivyo, hakuwa na bahati kwa sababu mama yake aliyekuwa kanisani kwa maombi, alimuona akitoka ofisi ya kanisa na kushuku kwamba alikuwa na uhusiano wa kimahaba na pasta. Kulingana na mdokezi, mama alipandwa na hasira na kuanza kumfokea mtu wa Mungu.

‘Kumbe wewe ni fisi mla kondoo!’ akalia mama huyo. ‘Unawezaje kumharibu binti yangu ilhali wewe ni mtu wa Mungu? Kumbe unafukuza mapepo ilhali **yamekuzonga**. Basi leo nitaondoa pepo la **uasherati** ndani yako linalokusumbua,’ mama aliwaka na kuchukua kipande cha mbao alichomwangushia pasta huku binti yake **akifyatuka kama risasi**. Kwa bahati nzuri pasta alimsukuma mama huyo akaanguka na kupata nafasi **kutimka** mbio kujiponya.

(*Taifa Leo*. Juni 8, 2014)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yaliyoulizwa.

Mke agawa mtoto wangu

Jina langu ni Boris Kigozi Nakeera. Ninaishi Kamwokya. Mimi ni mwanamziki na kwa hivyo wakati mwingi huwa safarini. Nina mchumba mmoja lakini karibu atanichosha mambo ya mapenzi. Miaka miwili iliyopita, mpenzi wangu huyu alipata mimba akajifungua na nikawa namshughulikia vilivyo.

Siku moja nilisafiri na mtoto wangu kwa wazazi wangu. Walipomuona walisema kuwa ni mtoto wangu bila shaka kwa sababu alikuwa ananifanana kila kitu. Sikuwa nimesikia tetesi zozote kuwa mke wangu lakini mwaka huu mambo yamenishtua.

Alianza kwa kuniambia kwamba alikuwa anataka kumpeleka mtoto kwa ndugu yake mtogo wa Kyebando amuone nami nikakubali. Baadaye nilianza kuona hali isiyo nzuri nyumbani. Wakati mwingine alikuwa akilala huko akinijulisha tu kuwa hangerudi. Nami sikuwa na shida kulihusu hilo. Mwezi uliopita tulipata sitofahamu

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Binadamu kwa wakati huu amemaka kwa sababu amechafua mazingira yake pasipo tahadhari. Mathalani insiya amejaza gesi za sumu zitokazo viwandani na hata kuchafua mito kutokana na maji machafu kutoka viwanda hivyo. Takataka zinazotupwa ovyo ovyo zinarundikana kila mahali. Isitoshe miti inakatwa vivyo hivyo bila simile. Matokeo ya haya yote ni kwa mfano tunapata mvua ya asidi ambayo huhasiri mimea. Aidha nao ukanda wa ozone unaotukinga dhidi ya miali hatari kutoka kwa jua umeharibiwa tayari na hivyo kuongeza joto duniani. sehemu nyingi zimeanza kugeuka na kuwa jangwa huku sehemu zingine zikifurika kwa maji ya mito na mvua. Maji haya yameanza kumeza visiwa vingi vilivyo baharini. Kutokana na madhara haya, binadamu sasa anatapatapa ili kutafuta makao kwingine kwenye salama. Ndiposa siku hizi nadhari za binadamu zimeelekezwa katika mawanda mengine nje kabisa ya kisayari hiki kidogo kiitwacho dunia.

Kwa miaka mingi sasa binadamu amekuwa akitafakari uwezekano wa kuishi katika sayari nyingine. Hii ndiyosababu mwaka wa 1969Waamerika walimkanyagisha binadamu wa kwanza kabisa mwezini. Lengo lilikuwa ni kutalii na kuchunguza uwezekano wa binadamu kuishi huko, wale watakaoweza wahamie huko. Kwa bahati mbaya iligunduliwa kwamba mwezini hakuna hewa wala hakuna kilicho hai huko, hata mimea. Mwezini ni vumbi tupu lisiloota cho chote. Kipatikanacho kwa wingi sana ni madini tu, ambayo hayawezi kumfaidi binadamu kwa lo lote.

Sayari nyingine alizozitalii binadamu ni Zuhura, Mirihi, Mushtara na tuseme karibu zote zinazolizunguka jua. kilichogunduliwa ni kuwa upo uwezekano wa sayari kama zuhura na pengine mirihi kuwa na mvua, lakini nyingi mno isiyoweza kuruhusu mimea kukua. Si tu, zuhura inasemekana kuwa joto sana wakati wa mchana ilhaliMirihi ni baridi sana siku zote; baridi kiasi cha kuwa binadamu na wanyama hawawezi kuishi huko. Mushtara yasemekana kuwa joto ajabu, ambapo hizo sayari nyingine zina joto sana au zina baridi sana. Habari hii imemfunga binadamu katika jela ya kijisayari chake kiki hiki kiitwacho dunia anachokichafua kila uchao.

Je, binadamu amekata tamaa? Hata kidogo! Ndio mwanzo anajaribu sana kuzikata pingu alizofungwa na maumbile. Vipi? Amejaribu kuchunguza uwezekano wa kuihama ardhi na kuishi baharini, kwa sababu bahari inazidi ardhi maratatu kwa ukubwa. Na ni vipi binadamu anadhani anaweza kuishi baharini mahali ambapo hakuumbwa aishi humo kama samaki? Jawabu ni kuwa angefanya hivyo kwa kutumia maarifa yake.

Binadamu anaamini kabisa kuwa ana uwezo wa kujenga miji mikubwa mikubwa humo humo baharini .... mikubwazaidi ya hii tuliyo nayo ardhini. Anaamini ya kuwa anaweza kuitawala bahari kiasi alichoitawala ardhi, na hivyo basikufanya bahari impe makao na kumlisha maumbile yake kwa kujiundiamashavu kwa mfano, ili avute pumzi ndani ya maji. Njia ya pili ya kuepukana na pingu za maumbile ni kuishi angani. Hii ina maana ya kujenga miji iliyoelea angani, kamamadungu vile. Na kwa vile anga haina kikomo, binadamu atakuwa amejipatia nafasi kubwa ya kuishi bila kujali ongezeko la idadi yake mwenyewe. Yaani atakuwa amejiundia visayari vyake visivyo idadi angani! Njia ya tatu ni kubadilisha umbo lake ili asihasirike na joto wala baridi. Binadamu wa kisasa anaamini kuwa inawezekana kumuunda upya mtu katika maabara badala ya katika mimba. Mtu huyu wa maabara, aitwaye 'cyborg'kwa lugha ya Kiingereza, anaweza kuwa na chuma ndani badala ya mifupa, na mwili wa kawaida wa dongo na maji nje.Kiunde huyu atakuwa hadhuriki ovyo ovyo kama binadamu wa sasa aliyeumbwa kwa chumvi, maji na protini. Au bora zaidi binadamu mpya wa maabarani aundwe kwa zebaki. Binadamu huyu wa zebaki hafi wala hakatikikatiki.

Ni iwapo atakatika vipande vipande, basi, kama zebaki, vipande hivyo vitaundika tena upya na kumrudishia umbo lake la awali kamili. Njia nyingi ya kuepukana na uangamizi ni kutumia viunde vyake vya elektroniki kama vile tarakilishi yaani kompyuta, na mitambo mingine kama hiyo. Binadamu anaamini kwamba uwezo wa vyombo hivi utakapokamilishwa, basi vitamsaidia kwa lolote lile.

**Maswali**

a) Inasemekana kwamba binadamu anakichafua hiki kisayari chake kila uchao. Kwa kutumia mifano miwili, eleza vile binadamu amechafua mazingira yake. (alama 2)

_____________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

b) Kwa nini ongezeko la joto limeleta jangwa duniani na wakati huo huo likaleta mafuriko? (alama 2)

_____________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

c) Eleza sababu mbili zinazomfanya binadamu kuhangaika na kutafuta makao kwingine. (alama 2)

_____________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

d) Ni mambo gani yanayomfunga binadamu katika ardhi. Taja mawili. (alama 2)

e) Unadhani ni kwa nini madini mengi yaliyoko mwezini hayaletwi duniani? Taja na ufafanue sababu mbili. (alama 2)

f) Kulingana na aya mbili za mwisho, eleza jambo ambalo binadamu anajaribu kukwepa. (alama 2)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)
mashavu

2. **MUHTASARI**
**Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Lugha ya Kiswahili ni lugha iliyoendelea sana. Leo hii lugha hii inasemwa na watu wote nchini Tanzania, Rwanda na
Burundi. Inasemwa na watu wote nchini Kenya. Nchini Uganda, Zaire, Malawi, Msumbiji, Zambia, Somalia,
Bukini (Madagascar) na Ngazija (Comoro), inasemwa na asilimia kubwa kubwa za wananchi wa huko. Aidha lughahii ina wasemaji si haba katika kisiwa cha Soktra na nchini Oman.
Fauka ya maendeleo haya, Kiswahili kinatumika kwa minajili ya matangazo ya habari katika idhaa nyingi za mashirika ya habari ulimwenguni. Nchi zenye idhaa za Kiswahili ni kama vile hizi zetu za Afrika ya Mashariki na Kati, Afrika ya Kusini,Nigeria, Ghana, Uingereza, (Shirika la B.B.C.), Marekani (Shirika la V.O.A.), Ujerumani (Shirika la Radio Deutch Well, Colgne), Urusi (Radio Moscow), China, India na kadhalika. Maendeleo mengine yanapatikana katika upande wa elimu. Marekani peke yake, kuna vyuo zaidi ya mia moja vinavyofundisha Kiswahili kama lugha muhimu ya kigeni. Huko Uingereza, vyuo kama London, Cambridge na Oxford vinafundisha lugha hii. Nchi nyingine ambazo zina vyuo vinavyofunza lugha ya Kiswahili ni kama vile Japan, Korea, Ghana, Nigeria na kadhalika.

Kweli Kiswahili kimeendelea jamani. Lakini je, kilianza vipi? Na ilikuwaje kikaweza kupiga hatua hizi zote? Kiswhaili kilianza kuzungumzwa \na kabila dogo la watu waliokuwa wakiitwa Wangozi. Watu hawa walikuwa wakiishi mahali palipoitwa Shungwaya. Shungwaya ni nchi ya zamani iliyokuwa eneo lililoko katika nchi mbili jirani ambazo siku hizi ni Kenya na Somalia. Kabila hili la Wangozi liliishi jirani na makabila mengine kama vile Wamijikenda, Wapokomo, Wamalakoe, (au Waelwana) na Wangazija (kabla hawajahamia visiwa vya Ngazija). Lugha ya Wangozi siku hizo, ambayo ndiyo mzazi wa Kiswahili cha leo, ilijulikana kwa jina Kiongozi. Kama ilivyosemwa hapo awali, kingozi kilisemwa na watu wachache sana. Je, lugha hii ilikuwaje mpaka ikapata maendeleo haya makubwa tunayoyashuhudua sikku hizi? Ama kwa hakika, Kiswahili ni lugha iliyobahatika tu. Inaweza kusemwa kwamba lugha hii ilipendelewa na mazingira na historia.

Jambo la kwanza, wageni waliotoka Mashariki ya kati kufikia hizi janibu zetu za Afrika ya Mashariki walikaribishwa vizuri na hawa Wangozi. Wakaingiliana wageni na wenyeji kindakindaki, kidini, kitawala, kibiashara na kitamaduni kwa jumla. Punde si punde, Wangozi, ambao baadaye walijulikana kama Waswahili na wageni hawa, wakaelimika katika dini (ya Kiisilamu), biashara na mambo ya utawala aina mpya. Lugha yao nayo ikapanuka pale ilipochukua msamiati wa kigeni hususan wa Kiarabu na Kiajemi na kuufanya uwe wake, ili kueleza kwa urahisi zaidi mambo haya mageni katika taaluma za dini, biashara, siasa na hata sayansi kama vile unajimu. Wakati huo, lugha ya Wangozi sasa ikaitwa Kiswahili wala sio Kingozi. Tatizo hapa ni kuwa kwa vile Kiswahili kilichukua msamiati mwingi wa kigeni ili kuelezea taaluma hizi mpya, baadaye kiimekujashukiwa kwamba ni lugha ya kigeni ilhali ni lugha ya kiafrika asilia, na kitovu chake ni nchi mpya za Kiafrika ziitwazo Kenya na Somalia hii leo.

1. **Soma kifungu cha habari hiki kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;-**

## MATATIZO NI SEHEMU MOJA YA MAISHA;-

Bibilia tukufu inasema kwamba Mungu alimuumba binadamu katika picha yake halisi. Inaaminika kuwa Mtu ambaye Mungu alimuumba kwanza ni Adamu. Na baada ya kuona kwamba Adamu alikuwa na upweke mwingi bila ya furaha, Mungu aliamua kumuumba Hawa ili aweze kumfariji na kumfurahisha katika maisha yake. Aliwapa maskani bora katika shamba la Edeni. Adamu na Hawa walikuwa na furaha tele maishani mwao kwenye shamba hilo. Lakini baada ya kufanya maovu na kumkosea muumba wao, Mwenyezi Mungu alikasilika sana akawalaani na kuwafukuza wote watoke kwenye shamba lake tukufu. Tangu siku hiyo, kila mwanadamu alilaaniwa na Mungu. Na hii ndiyo maana kuna matatizo na changamoto chungu nzima zinazomfuata binadamu kila usiku na mchana.

Tangu kuumbwa na kuzaliwa kwake, mwanadamu hupata mateso kadhaa na kumsababishia ugumu wa maisha. Zamani zile maisha yalikuwa matamu mithili ya asali ilhali maisha ya siku hizi ni machungu kama shubiri. Hii ndiyo sababu mwafaka inayoelezea kwanini watoto wachanga wanalia sana punde tu baada ya kutoka kwenye matumbo ya akina mama - wazazi wao. Wataalam wengi, yaani wajuzi wa mambo, wanasayansi pamoja na wanafalsafa wanasema kwamba mazingira mapya ndiyo yanayowasababishia watoto hawa wachanga kulia kwi!kwi!kwi! . Hata uzazi wenyewe ni mgumu. Lakini nilipowauuliza swali hilo mababu zangu wawili yaani; Mzee Bakidawo Kisitu na Jaajja Lujja Muteeweta, walinijibu kwamba; “watoto wachanga hawa wanalia kwa sababu huwa wameogopa matatizo na changamoto wanazozitegemea kuzipata hapa katika dunia au mazingira mapya”

Kila wakati, saa na dakika kuna mwanadamu anayekabiliwa au anayekumbwa na hali ngumu ya maisha. Dunia ni kigeugeu kama kinyonga au lumbwi! Dunia imebadilika sana na kila mabadiliko yanamuathiri mtu fulani . Miongoni mwa matatizo na changamoto kubwa wanazozipata wanadamu maishani mwao ni kama vile;-

Ugonjwa, kuna magonjwa sugu mbalimbali yanayotishia usalama na kushambulia afya ya binadamu na hatimaye kusababisha kifo; kama;- UKIMWI , Ebola, homa ya Malaria , nakadhalika..

Umaskini ni changamoto nyingine kubwa kwa binadamu. Maskini ni yule mtu duni ambaye hana uwezo wa kukidhi mahitaji yake msingi maishani. Asiye na mbele wala nyuma, hohe hahe!. Umaskini unatokana na mambo kadha wa kadha kama vile ; uzembe na uvivu, ukosefu wa ajira, Pamoja na ujinga wa mtu binafsi.

Njaa ni tatizo lingine kwa binadamu. Njaa ni ile hali ya ukosefu wa chakula cha kutosha. Maisha ya binadamu yanategemea chakula na bila ya chakula binadamu hawezi kuishi. Siku hizi kupata riziki au chakula ni vigumu hapa duniani kama kukwea mlima Kilimanjaro au Rwenzori. Na watu wengi wamekufa kwa sababu ya njaa. Uhaba ama ukosefu wa chakula mara nyingi husababishwa na mambo tele kama vile; ukame au uhaba wa mvua, udongo au ardhi isiyo na rutuba ya kuiwezesha mimea kukua vizuri, majanga makubwa kwa mfano dhoruba, ghalika au mafuriko( mvua nyingi) yanasababisha uharibifu mkubwa wa mashamba, mali pamoja na vifo vya watu.

Migogoro katika jamii ni changamoto nyingine. Hapa tunaona kwamba mwanadamu anapata na kupitia migogoro chungu nzima. Kama vile;- kugombana, kupigana, kurogana na kuuana. Vita vya wenyewe kwa wenyewe katika dunia hii vimesababisha vifo vya wanadamu wengi, kusambaratika kwa familia, ongezeko kubwa la wakimbizi, ukosefu wa usalama au amani na mdororo wa kiuchumi. Kwa mfano, hapa nchini Uganda kumekuwa na vita mbalimbali kwa mfano; vita vya kikundi cha waasi LRA wanaongozwa na Joseph Konny kule kaskazini mwa Uganda. Wananchi wengi huko wilayani Gulu,kitgum,Lira, Moyo, Pakwach nakadhalika, walipoteza mali pamoja na uhai wao vitani.

Mfano mwingine ni nchi ya Rwanda ambapo kulitokea vita vikali sana baina ya Wahutu na Watutsi. Marafiki , ndugu na majirani wote waliuana kwa sababu ya ukabira. Maelfu na maelfu ya watu walifariki dunia katika mauaji ya halaiki yaliyotokea nchini humo. Mfano wa pili ni nchi ya Kongo. Katika Jamhuri ya

kidemokrasia ya Kongo, watu wengi wamehama makazi au nyumbani kwao na kukimbilia usalama wao katika nchi jirani na wengine wameuawa vitani.

Kwa hivyo, kila mwanadamu anapitia mambo na matatizo au changamoto mbalimbali katika kukua kwake toka utotoni hadi ukubwani.

Hali na mfumo huo wa maisha utaendelea daima dawamu ama milele na milele. Tunamwomba Muumba Mwenyezi Mungu Mola Subhana Rabuka Allah aturehemu sana na kutusamehe madhambi yetu. Ameni.

**Maswali;-**

a) Pendekeza mada nyingine iliyo mwafaka kwa habari hii.
b) Mungu alimuumba mtu gani mwanzoni?
c) Mungu alikasilishwaje hadi akawafukuza Adamu na Hawa shambani Edeni?
d) Kulingana Bibilia, eleza sababu kwa nini binadamu anapata matatizo maishani mwake?
e) Kwa nini watoto wachanga wanalia wanapozaliwa?
f) Taja na uelezee mbinu au fani za lugha alizozitumia mwandishi katika habari hiyo.
g) Binadamu anakabiliwa na changamoto gani hapa duniani?
h) Eleza madhara ya vita vya wenyewe kwa wenyewe katika jamii.
i) Eleza maana ya vifungu vya maneno vifuatavyo;-
    i) changamoto chungu nzima.
    ii) Dunia kigeugeu
    iii) Asiye na mbele wala nyuma.
    iv) Maisha yalikuwa tamu mithili ya asali.
    v) Mauaji ya halaiki.

(i)**Tuvae Mavazi ya heshima**

Sisi wanadamu hatuendi uchi kama wanyama.Sisi huvuaa nguo,viatu,kofia,vilemba na mapambo mengineyo kama kila moja

wetu apendavyo .Mavazi yana muhimu mkubwa katika maisha yetu.Kwanza,mavazi hutusaidia kujikinga dhidi ya baridi au joto. Pili,mavazi hutusaidia kuficha sehemu nyingi za siri kwenye mili yetu.

Lakini siku hizi,vijana wengu hasa wasichaaa huvaa mavazi ambayo si ya heshima.wasichana wengu siku hizi atawakuta makivaa mavazi ambayo pamoja na kuwambana sana na hata yanaweza kuonyesha sehemu zao za siri za juu ya magoti.Baadhi ya wasichana huvaa nguo ambazo zinawesesha macho kupenyeza ndani yake na kuangalia mavazi ya ndani kama vile chupi au sidiria . Hata hivyo,wasichana wengine huvaa nguo ambazo zichanaa sehemu za migongo yao wazi kabisa . Mavazi kama haya ambayo yanaonyesha maumbile wazi wazi pamoja na sehemu za siri si ya hashima kulingana na utamaduni wa kiafrika.Jambo la kushangaza ni kwamba baadhi ya wana wake nao huvaa vivyo.Unamkuta mkwe wa bwana Fulani amevaa rinda ambalo pamoja na kumbana ,ni fupi sana.Hata akiwa anatembea ,mapaja yanaonekana wazi wazi huku matako yaliyobanwa na rinda hilo.yakibenukabenuka na kuonyesha pindo za chupi aliyovalia ndani ya rinda .

Kulitokea kisa kimoja kanisani cha kuaibisha sana .Msichana mmoja alikwenda kuhudhuria ibada ya jumapili huku amevaa rinda fupi sana na lenye kumbana barabara .Msichana huyo ambaye alikuwa mwanafunzi katika shule Fulani ya upili alifika baada ya ibada kuanza na hiyoiyeey akakaa kwenye viti vya nyuma.

Ibada hiyo ilikuwa maalum kwa sababu waliohudhuria waliombwa kushiriki katika ile sakramenti ya kukumbuka kufa Bwana Yesu Kristo.Na kwa hiyo aliwabidi waumini kwenda polepole kwenye altare na kupiga magoti mbele ya kasisi.Basi ,walikalia viti vya mbele ndio waliotangulia wakafuatiwa na wale wa wa viti vya katikati na mwishowe wale wa viti vya nyuma.

Zamu ya msichana huyo ilipofika ,yeye bila aibu yoyote akasimama na kwenda mbele kwenye altare ili apate ile sakramenti takatifu.Msichana huyo alipokuwa akipita katikati akielekea kwenye altare ,waumini wote walishanga sana kwa vile alivyokuwa amevaa nguo ya aibu hadharani .Rinda lilikuwa fupi sana kiasi kwamba mapaja ya msichana huyo yalikuwa yanaoneka wazi kabisa .Isitoshe hiyo ,rinda lake msichana huyo lilikuwa linambana sana hata alikuwa na matatizo kwa kutembea.Alikuwa akitembea .Alikuwa akitembea mfano wa mfungwa au mwendawazimu aliyefungwa kwa pingu miguuni.

Haya basi ,msichana akafika kwenye atare akajaribu kupiga magoti lakini akapata taabu.Akajaribujaribu na mwishowe akafaulu kupiga magoti likini kwa shida sana.

Lakini alipokuwa akingonja ili kasisi aje ampe kipande cha mkate pamoja na Mvinyo kama ilivyo kawaida ya sakramenti hiyo,waumini nyuma yake wakaanza kupiga makelele wakinungunika.

Wengine wakasema ,"Hapana, asipewe mkate na mvinyo!Hastahili hivyo.Yeye amekosa abadu."

Hata wanawake nao wakasema,"Hapana!Mavazi haya ya kisasa sasa yamevuka mpaka na kugeuka kitu kingine .Mbona yeye ameaibisha jamili ya wanawake"

Watoto ambao wao hawakujua ni aibu gani msichana alirusha,walikuwa wanacheta tu kwa kuwa wanachungulia chupi ya msichana huyo wakati alipokuwa akipga magoti.

Je, aibu gani iliyotokea,mpaka waumi wakapata kunungu'unika hivyo ? Ndugu yangu ,maajabu kweli yalitokea !Msichana Yule alipopiga magoti,rinda lake likaenda juu zaidi na kuacha matako yake wazi isipokuwa chupi aliyoivalia ndani.Ikawa aibu kubwa na mwanamume mmoja akasimama akamwendea Yule msichana akamkamata mkono akamvuta nje.Msichana alikuwa bado hajapewa bado hajapewa mkate na mvinyo.Kisa hicho kweli kiliiharibu ibada hiyo takatifu.Ndugu yangu ,ingawa tuna haki ya kuvaa kama vile tupendavyo,inatupasa kupasa kupasa kujiheshimu na kuvaa mavazi yenye heshima .Tuheshimu utamaduni wetu wa kiafrika ambao hauungi mkono mavazi yanayoonyesha sehemu za siri za mwili.Lazima tuvae mavazi ya heshima ,nasi tuwe na heshima.

**Jibu Maswali Yafuatayo**

1.Toa sababu tatu muhimu ukielezea umuhimu wa mavazi kwa binadamu.

2.Je,mavazi ambayo yanachukuliwa kama si ya heshma ni mavazi ya aina gani?

3.Fanyu utafiti na uandike sehemu zote za mwili wa binadamu.

4.Msichana anayezungumiziwa katika taarifa hii alikuwa amevaa vipi?

5.Kwa nini msichana huyo alikalia kwenye viti vya nyuma msichana alipopiga magoti kwenye altare?

7.Toa maelezo ya maneno yafuatayo=

(i) ibada
(ii) aibu
(iii) kasisi
(iv) mvinyo
(v) rinda
(vi) upindo
(vii) chupi

(viii) sidira
(ix) chungulia
(x) utamaduni